# KUKIMBIA KUTOKA KATIKA UPAGANI KWENDA KATIKA UISLAMU.

SWALI NA JIBU.

Kwa jina la Mwenyezi Mungu na kila sifa njema zina mstahiki Mwenyezi Mungu na Rehema na amani ziwe juu ya Mjumbe wa Allah na kwa watu wake na Masahaba zake, na wale watakao mfuata, Na baada ya hayo:

Kitabu hiki Kidogo: (Kukimbia kutoka katika upagani kwenda katika Uislamu).

Kinatoa kijitabu hiki uwazi wa "Tabia ya upagani" na utata wake, na ni jinsi gani upagani (Upingaji) unavyopingana na mambo ya kawaida kiakili na kimaumbile.

Na kinaweka wazi kijitabu hiki baadhi ya hoja zinazo thibitisha kuwepo kwa Muumbaji Aliye takasika.

Kwa hivyo sisi tunamjua Mwenyezi Mungu kupitia akili, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu. "Je, wameumbwa bila kutokana na kitu chochote, au wao ndio waumbaji". Suratu Tuur: 35.

Kwa akili ya kawaida, hapa inategemea mambo matatu na hakuna la nne yake:

Jambo la kwanza: Ima tuwe tuliumbwa bila muumbaji, kwa kauli yake " Je, waliumbwa bila kutokana na kitu chochote) na hili haliwezekani, yaani inawezekana vipi tuumbwe bila Muumbaji?

La pili: Au tuwe tumejiumba wenyewe, kwa kauli yake "Au wao ndio wamejiumba" na hili haliwezekani pia, kwa sababu inawezekanaje nijiumbe mwenyewe kabla sijaumbwa?

Hivyo, kwa akili ya kawaida unabakia uwezekano wa tatu ambao Aya imenyamaza haikuuzungumza, kwani unafahamika wazi hata bila kwenda shule, nao ni kuwa tunaye muumbaji aliye tuumba.

Hivyo, sisi tunamjua Mwenyezi Mungu kupitia akili.

Na hivyo hivyo sisi tunamfahamu Mwenyezi Mungu kupitia maumbile.

Na tunaelewa kupitia maumbile yetu kuwa masanamu na tabia ya asili havimiliki uwezo wa kuumba ulimwengu wala kumleta bakteria mdogo wala mwanadamu, wala kudhibiti kazi za mwili wa mwanadamu kwa sura ya namna hii, wala kuumba kwa ufanisi kutoka punje hadi kufikia kuwa Sayari.

Masanamu wanayo yaabudu Makafiri, na tabia ya asili wanayoiamini wapagani (wasoiamini uwepo wa Mungu) vyote viwili vinahitajia kutoka kwa muumbaji wake.

Masanamu wala tabia ya asili havimiliki lolote katika mambo yake, na wala havina uwezo wa kudhibiti homoni zilizoko ndani yako. kwa kiwango hiki cha kutisha, wala havina uwezo wa kuweka uwazi wa sehemu ya uzazi ambao ndani yake kuna mamiliona ya elimu ndani ya kila seli, wala havina uwezo wa kukileta kitu chochote, wala hata kujileta vyenyewe haviwezi.

Muumbaji ndiye mjuzi wa maajabu haya, naye ni muumbaji Mtukufu Mjuzi Muweza, Mfanisi Aliye takasika.

Kisha kijitabu hiki kinakwenda kujadili baada ya hayo, Utata wa wapagani, na majaribio yao ya kuzidhoofisha hoja za kiakili na za kimaumbile za uwepo wa Muumbaji.

Na miongoni mwa Uongo wao mashuhuri ni kauli yao kuwa: "Ulimwengu ulitokea tu ghafla", na hii ni kwa sababu ya kuto kuelewa kwao au kwa sababu ya kupuuza kwao misingi ya majibu yanayoweza kujitokeza kichwani; kwa sababu jambo la ghafla huwa lina sababu mbili ambazo ni lazima ziwepo.

Ambazo: Ni wakati na Mahali.

Jambo la ghafla ni sharti ndani kuwe na muda ambao tukio hilo lilileta athari zake.

Na ni sharti pia kuwe na malighafi mahali ambazo zitaleta matokeo ya kitendo kilicho kusudiwa.

Inawezekanaje tuamini kuwa ghafla imeuleta ulimwengu, hali yakuwa imetokea bila muda wala sehemu, tena bila ghafla!!.

Kisha kijitabu kinaleta baadhi ya dalili au ushahidi wa kiakili wa kuonyesha ulazima wa kuwepo Dini, na maana ya Dini, na ulazima wa kujisalimisha kwa Mola Mlezi wa walimwengu na kumtii yeye Mtukufu.

Kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na kumtii yeye kwa kutekeleza amri zake, Na hii ndio maana halisi ya Dini.

Wewe unatakiwa kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, na umuabudu muumba wako, na anaye kupa riziki, na anakupatia kila aina za neema na zawadi.

Hivyo basi Ibada ni haki ya Mwenyezi Mungu kwa Waja wake,kwa kuwa yeye kutakasika na machafu ni kwake ambaye ametuumba na akatuo\pa Uhai na akatuongoza na akaturuzuku na akatutumia Mitume wakeili atupime na kutujaribu kuwa nani miongoni mwetu atakuwa ni mwenye kutenda matendo Mema,Hivyo basi Ibada ni Haki ya Mwenyezi Mungu iliyokuwa wajibu kwetu sisi. "Aliyeumba mauti na uhai ili awatahini nyinyi, enyi watu, ni yupi miongoni mwenu aliye mwema wa matendo na utakasaji wa nia? Na Yeye Ndiye Mshindi Ambaye hakuna chochote kinachomshinda, Ndiye Mwingi wa msamaha kwa anayetubia miongoni mwa waja Wake" Suratul Mulk. Kisha katika sehemu inayo fuata kinatoa kitabu

baadhi ya ushahidi juu ya usahihi wa uislamu, na kubainisha uhakika kuwa Mwenyezi Mungu hakubali kwa watu Dini yoyote zaidi ya Uislamu, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu. "Na Mwenye kutafuta Dini isiyokuwa dini ya Kiislamu, basi hiyo haitakubaliwa kwake, na yeye Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye kupata hasara". [Surat Al Imrani: 85]
Uislamu ndio Dini aliyo watuma kwayo Mwenyezi Mungu Manabii na Mitume wote.
Na nembo kuu ya uislamu nikuwa: Ndani yake kuna maana ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake.
Na uislamu ndio sheria kamilifu zaidi kuliko zote, inahimiza kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu.
Na ndio Dini ya pekee inayo waita watu kumpwekesha Mwenyezi Mungu, Tauhidi ambayo walikuja nayo Manabii wote.
Manabii wote walikuwa katika Tauhidi, hata kama zitatofautiana sheria zao.
Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na hatukupata kutuma kabla yako, ewe Mtume, mjumbe yeyote isipokuwa tunampatia wahyi kwamba hapana mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu. Basi mtakasieni Ibada Yeye Peke Yake". Suratul Anbiyaa: 25
Na haijabakia katika tauhidi hii Dini yoyote zaidi ya uislamu katika mgongo wa Ardhi, kwani wote wenye kujinasibisha na sheria zingine, wamekuwa na fungu sawa sawa liwe dogo au kubwa, baada ya kufa manabii na baada yakuwa wamewaacha watu katika imani ya kumuabudu Mungu mmoja (Tauhidi) watu wakajifanyia ushirikina, na mpaka leo hii hakuja aliyebakia katika Tauhidi safi waliyo kuja nayo Manabii Dini yoyote zaidi ya uislamu.
Kisha kinahitimisha kijitabu hiki kwa kuweka wazi ni namna gani mtu anaweza kuwa muislamu, na maana ya uislamu, na udharura wa uislamu.
Uislamu umejibu maswali yote ya uwepo yanayo zunguka katika kichwa cha kila mwanadamu: Tulitokea wapi? Na ni kwa nini sisi tuko katika ulimwengu huu, Na tunakwenda wapi baada ya hapa?
Uislamu umeyajibu haya yote katika aya moja tu katika Qur'ani Tukufu, Amesema Mola wetu Mlezi Aliye takasika na kutukuka. «Na ni kitu gani kitakachonizuia mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu Aliyeniumba na Ambaye Kwake mtarejea nyote?" Suratu Yasin.
Ulitokea wapi? Mwenyezi Mungu ndiye aliye niumba.
Na ni wapi nitakwenda mimi? Nitakwenda kwa Mwenyezi Mungu ili nihesabiwe kwa matendo yangu. "Na kwake mtarejeshwa".
Kwa nini nilikuja katika dunia hii? Kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu na ili nipewe mitihani.
Kwa nini namuabudu Mwenyezi Mungu? Ni jambo la kawaida mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu aliye niumba, hii ni tabia ya mahusiano baina ya mja na Mola wake, kuwa mja amuabudu Mola wake na muumba wake. «Na ni kitu gani kitakachonizuia mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu Aliyeniumba?" Aya moja imekusanya majibu ya maswali matatu muhimu yanayo washinda Binadamu kuyajibu. «Na ni kitu gani kitakachonizuia mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu Aliyeniumba na Ambaye Kwake mtarejea nyote?" Suratu Yasin: 22.
Uislamu ndio sheria ya Mwenyezi Mungu kwa ulimwengu mzima.
Na uislamu una maanisha ni mtu aisalimishe nafsi yake kwa Mwenyezi Mungu, amnyenyekee Mwenyezi Mungu na atii sheria zake, na ajishushe kwa muumba wake na Mola wake.
Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu "Na mwenye kumtakasia Mwenyezi Mungu ibada yake na kumkusudia kwake Mola wake Aliyetukuka, na akawa mwema katika maneno yake, mwenye kutengeneza matendo yake, basi huwa ameshikamana na Kamba iliyomadhubuti kwenye radhi za Mwenyezi Mungu na Pepo Yake". Suratu Luqman: 22 Uislamu una maanisha utumwa kwa Mwenyezi Mungu katika kila dogo na kubwa katika maisha yako, Amesema Mtukufu. "Sema, ewe Mtume, kuwaambia hawa washirikina, «Hakika Swala yangu na nusuk yangu, yaani kuchinja kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Peke Yake; Pia uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe wote". «Asiye na mshirika katika uungu Wake wala katika Umiliki Wake wala katika Majina Yake na Sifa Zake. Kumpwekesha huko Mwenyezi Mungu kulikosafishika ndiko Alikoniamrisha mimi Mola wangu, Aliyetukuka na kuwa juu. Na mimi ni wa kwanza kumfuata Mwenyezi Mungu kikamilifu katika umma huu.» Suratul An-am: 162-163.
Swala zangu na Vichinjwa vyangu na Uhai wangu na Mauti yangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu: Kila kitu ninakifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mimi nina swali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na nina watii wazazi wangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na ninarejea masomo yangu na kujifunza ili niwanufaishe watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na nina lala ili nipate nguvu kesho ya kufanya yale aliyo niamrisha Mwenyezi Mungu.
Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu katika kila jambo, na hii ni katika alama muhimu ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu.

Njaa ya maarifa: Yaani: Njaa ya kupata maarifa ya mambo muhimu yanayo tushughulisha, hakuna kinachoweza kuishibisha zaidi ya uislamu.
Wakati ambao upingaji (Upagani) hauna majibu kwa mtu zaidi ya kuambiwa kuwa alizaliwa ili afe!.
Kijitabu kinatoa mafunzo: Zoezi la vitendo na akili kuhusiana na maswali tata ya upagani, na baadhi ya ushahidi wa usahihi wa uislamu.
Zoezi liko katika mfumo wa swali na jibu.
Haya, Tuanze kwa baraka za Mwenyezi Mungu!.

## 1- Nini maana ya upagani?

Jawabu: Upagani: Ni kukataa kuamini kwa namna yoyote ya mambo yasiyoonekana.
Mpagani hupinga uwepo wa muumbaji, na utume, na kufufuliwa.

## 2- Ni kitu gani mnacho kiona ni dosari katika upagani?

Jawabu: Upagani una maanisha imani ya juu zaidi ya Dini.
Lakini ni imani iliyo jengeka juu ya mawazo na dhana, na fikira zisizo sahihi, kinyume na imani ya dini iliyo jengeka kwa mambo akili ya kawaida ya kimaumbile, na mambo ya uhakika tunayo yaona kwa macho yetu, na mambo kiakili, na hoja za kisheria.
Ili uanze kupinga unatakiwa kujiuliza yafuatayo: (a) Hapakuwa na kitu halafu paka ungana na kitu na hatima yake kikawa kitu kikubwa! Ukawa ulimwengu wa kutisha tena mzuri zaidi tena kwa viwango vya juu kabisa na mipaka iliyo jaa misitu. (b) Ghafla imezaa mipaka yenye misitu na Nishati ambazo ndizo zilizo tengeneza ulimwengu; lakini wakati huo huo sharti la kutokea kitu ghafla ni kuwe na mahali na wakati wa kutokea tukio, na ulimwengu ulizuka tu bila mahali wala wakati, ndiyo maana ulizuka ghafla!
Jawabu: Bila mpangilio pamoja na mazingira ya ardhi ya mwanzo ndivyo vilivyozalisha maisha na vikaanzisha bakteria pamoja na wanadamu, na wakati huo huo akili ya mwanadamu kwa ukaidi wake na ujeuri wake haiwezi kuzalisha taswira ndogo ya maisha. (c) Maadili na tabia njema zote ambazo tunakubali kuwa ziko sahihi ambazo nyingi zinaelekea katika kupinga swala la kiini (asili) kabisa, Maadili ya asili (Yasiyo na mwanzo) husababisha mzigo mkubwa na hasara kwa kiwango cha kuharibu masilahi ya ulimwengu, na hii ni miongoni mwa vitu ambavyo kiini kinazalisha chenyewe. Sasa mambo haya yasiyo ingia akilini unatakiwa kuyaamini kwanza ili uanze kupinga!.
(d) Haipatikani hoja ya kiakili wala ya kuonekana katika upagani inayo zuia kuangamizwa watu wote wa ardhini.
Pia ulimwengu wa kuamini vinavyo onekana haujui kosa na usahihi ni upi?
Hivyo, ni sawa tu watu wote kuangamizwa kwa kuwahuisha, kwa mujibu wa fikira za kipagani.
Upagani umejengeka katika imani pia, lakini ni imani isiyokuwa na athari yoyote ya kielimu au nukuu au akili au tabia.

## 3- Ni upi ushahidi wa kuwepo kwa muumbaji?.

Jawabu: Ushahidi ni mwingi lakini tutosheke na hizi mbili.
1- Ushahidi wa kuleta (Kuumba)
2- Ushahidi wa kutilia umuhimu na ufanisi.

## 3- Nini maana ya ushahidi wa kuleta?

Jawabu: Ushahidi wa kuleta yaani: Nikuwa:
Kila kitu kilichozushwa, yaani, kimepatikana baada ya kutokuwepo, hii inamaanisha ni lazima awepo aliye kizusha, Yaani: Aliye kifanya kiwepo.
Na kupitia hili tunakuwa na ushahidi mwingi usio hesabika wa kuwepo muumbaji Mtukufu.
Kila punje katika ulimwengu ni alama juu ya uwepo wa muumba, kwani kila kitu kilichozuka na kikaonekana kuwepo ni dalili juu ya muumbaji aliyepwekeka
Hata wewe ukitazama katika vitu vilivyopo itakubainikia kuwa vilizuka (havikuwepo) na vina mabadiliko na si vya kudumu au vya milele, na vile vile pia havijajitosheleza vyenyewe, na hii inakufanya uelewe mwenyewe kwa akili yako kuwa hivi vinamuumbaji, Na hapo utabadili mtazamo wako kuwa kuna aliyeuleta ulimwengu, kwa kutazama pekee katika ulimwengu.
Na kwa ajili hii ni mara ngapi aya za Qur'ani zimeangazia ulimwengu, na vilivyomo ndani yake, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Sema, ewe Mtume, kuwaambia watu wako, «Fikirini na mzingatie kwa yaliyomo mbinguni na ardhini miongoni mwa aya za Mwenyezi Mungu zilizo waziwazi.» Lakini aya, mazingatio na Mitume wenye kuwaonya waja wa Mwenyezi Mungu adhabu Yake, vyote hivyo havikuwa ni vyenye kuwanufaisha watu wasioamini chochote katika hivyo, kwa sababu ya kupa mgongo kwao na ujeuri wao". Surat Yasin. Na amesema Allah Mtukufu: "Kwani hawakufikiri, (hawa wakanushaji Mitume wa Mwenyezi Mungu na kukutana na Yeye), vile Mwenyezi Mungu Alivyowaumba, na kuwa wao

Amewaumba na hawakuwa kitu chochote? Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yake isipokuwa ni kwa ajili ya kusimamisha uadilifu, malipo mema na mateso na kutolea ushahidi upweke Wake na uweza Wake. Na kwa muda uliotajwa wa kukomea kwake nao ni Siku ya Kiyama. Na kwa hakika, wengi wa watu ni wenye kukataa na kukanusha kwa ujinga wao wa kutojua kuwa marejeo yao ni kwa Mwenyezi Mungu baada ya kutoweka kwao na kwa kughafilika kwao na Akhera. Suratu Rum. Na alisema Allah Mtukufu: "Au kwani hawaangalii, hawa wakanushaji aya za Mwenyezi Mungu, kwenye ufalme wa Mwenyezi Mungu uliyo mkubwa na mamlaka Yake yenye uwezo wa kushinda, mbinguni na ardhini na chochote kile Alichokiumba Mwenyezi Mungu,na huenda ukawa umesogea karibu wakawa watakufa kwenye ukafiri wao na watakuwa kwenye adhabu ya Mwenyezi Mungu na mateso yake makali? Basi ni kitisho gani na onyo gani baada ya onyo la Qur'ani wataliamini na watalifanyia kazi?" [Suratul A'raf: 185]
Kila kitu kilichozushwa ni: kielelezo cha wazi cha mletaji wake!

# 5- Nini maana ya ushahidi wa kujali na ufanisi?

Jawabu: Ushahidi wa kujali na ufanisi: N ikuwa:
Kila kitu duniani kwa ujumla kwanzia seli ndogo zaidi mpaka katika vitu vikubwa, vyote hivi kila kimoja kinabeba sehemu miongoni mwa sehemu za mahusiano, katika kazi zake.
Yaani: Kila kimoja kinatimiza kazi yake maalumu na jukumu pekee. (Lisiloingiliana na jukumu la kitu kingine)
Na kila mafungamano ya utendaji kazi katika asili yamepangiliwa kwa kitendo cha uwepo wa kitu husika. Na uwepo wake pia umepangiliwa.
Na mafungamano ndani ya uwepo wa kitu pia yamepangiliwa kwa kitendo cha uwepo wa kitu husika.
Kila kinachokuzunguka kimesanifiwa kwa namna maalumu ili kiweze kutimiza kazi iliyopangwa.
Hivyo basi, kila kinachokuzunguka kimebeba mafungamano ya utendaji.
Na mafungamano ya utendaji kazi ndiyo alama ya kutengenezwa na kupatikana.
Hivyo, lazima kuweko aliye kileta.
Mfano wa hilo: "Taa" Hii inatoa mfano mzuri wa mafungamano ya kiutendaji.
Taa ya umeme inatengenezeka kwa:
Fyuzi.
2- Waya wa Madini ya Shaba: Unaopeleka umeme katika fyuzi.
3- Gesi hafifu: Inayo linda fyuzi, na wala haihusiki na fyuzi wala umeme wenyewe.
4- Kioo: Kinachozuia hewa kuingia au gesi hafifu kutoka nje, vinginevyo fyuzi ingeungua.
5- Kanuni ya Taa: Taa huunganishwa kwa nyaya zenye gamba na kuwa ndio mapitio ya nishati ya umeme.
Hapa Taa tunaiita kuwa ndio mfumo wa mafungamano haiwezekani kuieleza zaidi ya hapo, na hapo kuna ushahidi wa kiakili wa utekelezaji wa ufundi huu wa kifanisi.
Mtu anaye pinga ufundi huu wa kifanisi wa Taa, au akawaza kuwa ilitokea tu yenyewe ghafla (pasi nakuwa na fundi), huyu ndiyo anatakiwa atupe ushahidi wa haya anayo yasema!
Aliyetengeneza Taa anajua vizuri maana ya umeme, na njia zake na faida za Taa, na hisia (sensor) za fyuzi, Hivyo kuwepo kwa Taa ni dalili ya moja kwa moja ya kuwa ina fundi wake mfanisi, na wala si aina zisizokuwa na mpangilio (ambazo hazikutengenezwa) eti kwa kuwa kuna aina nyingi ya Taa tofauti tofauti zilizo katika muundo wake kamili!.
Na kiwango hicho hicho cha kutoa ushahidi wa kiakili tunaona kuwa kitu chochote kilichowekewa mafungamo ya kiutendaji mfano kama Mwanadamu, yuko aliyemfanya kuwepo.
Taa inatengenezeka kwa vifaa vitano. (Hii tunaamini kuwa inamtengenezaji wake!)
Wakati huo huo, Mwanadamu amekusanya vitu Bilioni nne (4) katika kila seli miongoni mwa seli zake.
4- Mchanganyiko wa vitu Bilioni nne, vyote hivi vinasimamia kazi kwa kiumbe hai, ambazo huitwa seli au (DNA) (vinasaba) na seli hizi hukaa katika kila uwazi miongoni mwa uwazi wako.
Kwa akili ya kawaida, ikiwa utakubali kuwa vifaa vitano (5) vinavyotengeneza taa vina fundi wake aliye vitengeneza, halafu wewe huna fundi aliye kutengeneza, basi hili litakuwa ni tatizo lako mwenyewe!.
"Je, wameumbwa bila kutokana na kitu chochote, au wao ndio waumbaji". Suratu Tur: 35.
Na kila kitu kinachokuzunguka kina mafungamano, na hakipatikani kitu katika asili wala katika punje wala katika anga wala ndani ya mwili wako kisichokuwa na mafungamano ya kiutendaji kabisa.
Mafungamano ya kiutengaji, na kazi ya kila punje ndogo, na seli zote ni vitu vinavyopatikana katika kila kitu katika ulimwengu.
Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu "Hakika, katika kuumba mbingu kwa kuzifanya ziinuke juu na ziwe kunjufu, na ardhi kwa majabali yake, mabonde yake na bahari zake, na katika kutafautiana usiku na

mchana kwa urefu na ufupi, giza na muangaza, na kuandamana kwao kwa kila mmoja kukaa pahali pa mwingine, na katika majahazi yanayopita baharini, yanayobeba vitu vinavyowanufaisha watu, na katika maji ya mvua Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kutoka mbinguni, Akaipa uhai ardhi kwa maji hayo ikawa rangi ya kijani yenye kupendeza baada ya kuwa kavu isiyokuwa na mimea, na vile Alivyoeneza Mwenyezi Mungu humo kila kitambaacho juu ya ardhi hiyo, na katika yale Aliyowaneemesha kwayo ya kuugeuza upepo na kuuelekeza, na katika mawingu yanayopelekwa baina ya mbingu na ardhi, hakika, katika dalili zote hizo zilizopita, pana alama za upweke wa Mwenyezi Mungu na ukubwa wa neema Zake kwa watu wanaoelewa sehemu za hoja na wanaozifahamu dalili za Mwenyezi Mungu Aliyetukuka juu ya upweke Wake na kustahiki Kwake Peke Yake kuabudiwa". Suratul Baqara.

Na Aya katika hilo ni nyingi mno;

Na hawezi kuzingatia na kukumbuka ila mwenye kutumia akili yake. "Na hawazingatii ila watu wenye akili" [Surat Al Imrani: 85]

Atakayetumia akili yake na akatazama ulimwengu (Kwa kutafuta ushahidi wa kuumbwa kwake) na akatazama kupangiliwa kwa kazi za vilivyopo (Ili kupata ushahidi wa kuendeshwa na ufanisi wa vitu hivi) Moja kwa moja atajiridhisha kuwa yupo aliyevifanya viwepo, kwa akili ya kawaida!

# 6- Kwa nini asiwe mwanadamu na viumbe vinginevyo vyanzo vyao vya mwanzo ni malighafi ndogo kabisa?

Jawabu: Hapa kuna matatizo mawili:

Tatizo la kwanza: Nikuwa hakuna ushahidi wa wazi unao onyesha kuhama kwa aina moja ya kiumbe hai na kuwa kiumbe kingine, achilia mbali kipengele hiki cha dhana ya kuwa mwanadamu amepatikana mwanzo kutokana na kiumbe kingine.

Mpagani ana amini vipi dhana hii isiyowezekana, na kwa ushahidi gani wa wazi, na anatupinga ushahidi wetu wa kiakili wa dini?

Tatizo la pili: Kulingana na nadharia ya kiumbe kidogo kabisa cha mwisho (Minimum gene set concept) haiwezekani kwa kiumbe hai chochote kwa namna yoyote ile kitakavyokuwa kushuka chini ya kiwango cha (gene/cistron) (vinasaba) mia mbili (200)

Na kiwango cha chini kabisa cha jeni (vinasaba) ni kile kiwango cha mwisho ambacho hakuna kiumbe kinaweza kuwa hai chini ya hapo!.

Hakuwezi kuwa na kiumbe hai ikiwa idadi ya jeni itapungua chini ya kiwango cha mwisho kwa kiasi cha jeni moja.

Jeni: Ni mfumo maalumu kwenye seli za kiumbe hai ambayo hukipa kiumbe hicho sifa za kimaumbile na hurithishwa na wazazi.

Kuna kiwango maalumu cha lazima cha Jeni kwa ajili ya uhai kiasi kwamba, hujikusanya kundi la jeni hizi kwa ajili ya kutengeneza nguvu, kwa sababu hakuna uhai wa kiumbe hai bila kuwa na nguvu, na kundi jingine la jeni hujikusanya kwa ajili ya lishe, na jeni zingine hujikusanya kwa ajili ya kutengeneza wingi, na zingine hujikusanya kwa ajili ya kazi zingine muhimu za maisha, na zaidi ya hapo!.

Walifanya utafiti wasomi wakubwa wa kiwango cha chini kabisa cha Jeni cha lazima kwa ajili ya uhai, na wakapitisha kuwa haiwezekani kupungua chini ya Jeni mia mbili.

Na Taasisi ya Craig venter ilitoa matokeo kuwa kiwango cha chini kabisa cha Jeni hakipungui chini ya Jeni mia tatu themanini na mbili (382)[1]

Na waligundua wana sayansi kuwa (Bakteria aina ya) Mycoplasma ndiye kiumbe mdogo zaidi kuwahi kupatikana ulimwenguni kote, lakini ana Jeni mia nne na sitini na nane (468).

Na jambo lingekuwa ni kiini tu, na ulimwengu ni utaratibu wa kiini pekee, basi hapo sisi tutakuwa na haja ya kuanza na Jeni sifuri, tukitaka kupita kutoka katika hydrogen mpaka kufikia kuwa binadamu!.

Lakini sayansi inatueleza kuwa hakuna kitu kinaitwa Jeni sifuri,Au Jeni moja,Au hata Jeni mia moja (100)

Sayansi inasema: Hakika sisi tuna haja kubwa ya kuwa na kiwango kikubwa cha takwimu (data) zinazo onyesha kiwango cha chini zaidi,Na vinginevyo kisingetokea kiumbe hai kwanzia mwanzo.

Hivyo hakuna kitu katika asili ati kimetoa mwanzo ghafla na hakikuwepo,Bali kila chenye mfumo na mpangilio kilianza kwa hatua za mabadiliko ya mustakabali wake!.

Na hatua za mabadiliko zitaendelea katika mfumo wa data (takwimu) ambazo hukusanywa kabla ya kiumbe kudhihiri,Na yataendelea mabadiliko haya milele kuwa ni jiwe zito katika uso wa wapagani,Na jiwe zito wapingaji wa uumbaji wa Mola!

---

[1] J. Craig Venter Institute (JCVI) conducted a study to find all the essential genes of M. genitalium through global transposon mutagenesis. As a result they found that 382 out of 482 protein coding genes were essential.

Sasa hivi wewe uko mbele ya data (Takwimu) maalumu bilioni nne (B.4), data hizo zinazopatikana ndani ya kila kiini cha seli miongoni mwa seli zako, kwa ajili ya kuzalisha kazi hai na nyeti kwa ajili ya maisha. Mpagani alikuwa na dhana yakuwa kuna kiumbe kilicho anza na Jeni sifuri, Lakini ikaja nadharia ya kiwango cha chini cha Jeni ikaimaliza ndoto hii.
Kiumbe hai kilidhihiri kikiwa kimefungamanishwa na kazi zake tangu kuonekana kwa mara ya kwanza,Na laiti isingelikuwa hivyo basi,Kisingelikuwepo tangu mwanzo.

# 7- Ni ipi mifano ya kuonyesha ushahidi wa kutilia manani na ufanisi?

Jawabu: Mifano haina idadi.
Na hayawezi kuitosheleza mafaili yote ya ardhini.
"Na lau miti ya ardhi yote ingalichongwa ikafanywa kalamu na bahari ikawa ni wino wake, na zikaongezwa juu yake bahari saba, na yakaandikwa, kwa kalamu hizo na wino huo, maneno ya Mwenyezi Mungu yatokanao na ujuzi wake na hukumu Zake na yale ambayo Amewaletea wahyi Malaika Wake na Mitume Wake, zingalivunjika- vunjika kalamu hizo na ungaliisha wino huo, na hayangaliisha maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia ambayo hakuna mwenye kuyazunguka kiujuzi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mshindi Mwenye nguvu katika kuwatesa wanaomshirikisha, ni Mwingi wa hekima katika kuendesha mambo ya viumbe Vyake. Katika aya hii pana kumthibitishia Mwenyezi Mungu Aliyetukuka sifa ya Maneno kikweli, kama inavyonasibiana na utukufu Wake na ukamilifu, kutakasika na sifa za upungufu ni Kwake". Suratu Luqman: 22
Kila punje katika ulimwengu ni kielelezo cha kutiliwa manani, sawa tuuelewe uhakika huo leo au kesho.
a- Insulini -Ni homoni za kumeng'enya glukosi (sukari) huzalishwa na (Pancreas) kongosho kutokana na kiwango cha sukari ulicho kula.
b- Nguvu ya moyo kusukuma damu inaendana na nguvu ambayo viungo vinaihitaji kulingana na juhudi zinazotumika.
c- Mifuniko ya utumbo wako inayofanya chakula kisirudi mdomoni mwako ukaudhika kwa hilo
d- Mifuniko ya sehemu za kutolea,Inayozuia uchafu usikutoke ili nguo zako zisichafuke kila wakati.
e- Mifupa ya fuvu la kichwa chako huwa haioti nyama mpaka utoke ndani ya tumbo la mama yako ukiwa salama tena kwa urahisi na wepesi, kwa sababu laiti ingelikuwa na nyama basi usingeweza kushuka kutoka tumboni mwa mama yako ila baada ya kuivunja mifupa hiyo,Na wala mifupa hiyo haikamilika kukua kwake mpaka kukamilike kukua kwa ubongo wako.
f- Na kila mshipa wa viungo vyako ambao husafirisha nishati ya umeme umefunikwa kwa mfuniko wa uzio (Insulator), kama tunavyo fanya sisi leo hii katika nyaya za umeme, ili nishati ya umeme isipenye na kuchanganyikana au kupotea au ikakusababishia usumbufu.
g- Umeme huzunguka katika kiini (Nucleus) kwa kasi ya kilomita elfu moja (1000) kwa sekunde na vinginevyo basi inge dondoka katika kiini hicho, kwa sababu ya nguvu ya mvutano iliyoko katika kiini kinachozalisha umeme,Na ulimwengu unge poromoka kabla hata ya kuanza,Na hii ndiyo kasi ya mfano mdogo wa kutengenezeka kwa punje ndogo.
h- Chembe mbili zinapo zungukwa na Hidrojeni basi asilimia 0.007% ya kundi la Hidrojeni hubadilika na kuwa nishati (nguvu), na laiti kundi hili lingelikuwa ni asilimia 0.006% badala ya 0.007% basi protoni (Sehemu ya kiini cha atomu chenye chaji chanya) haitoweza kushikana na nyutroni (Neutron), na hapo basi ulimwengu ungeendelea kubaki kuwa Hidrojeni pekee, na vipengele vingine visingetokea vyanzo vyake, na laiti kama ingekuwa kundi linalobadilika na kuwa nishati ni 0.008% badala ya 0.007%, basi mzunguko ungelikuwa mkubwa mno, jambo ambalo litasababisha kupotea kwa Hidrojeni kwa haraka mno katika ulimwengu, na maisha yasingewezekana kuwepo kwa hali hiyo, hivyo namba inalazimika kuwa kati ya 0.006% na 0.008% yaani isishuke wala kupanda juu zaidi ya 0.007%.
i- Mkusanyiko wa umeme (Electron mass) huwa 0.2% katika mkusanyiko wa nyutroni (Neutron mass), na huu ndiyo mfano wa kipimo cha kutengeneza chembe (punje) moja.
j- Vichipuzi huelekea upande wa mwanga mara tu vinapoanza kuota, na mizizi huelekea upande wa chini kiasi ambacho vichipuzi hufurahia kuakisi mwanga wa jua kali, na kila malighafi inayohitajika kwa ajili ya kusimamia utendaji kazi wake hupatikana ndani ya kuta za mbegu, na kuna homoni zinazoendesha ukuaji wa kwenda juu na wa pembembeni (matawi) wa mmea, na upande wa mizizi pia, na yote hiyo iko ndani ya kuta za mbegu.
k- Wakati unapokula tunda tamu kisha ukatupa mbegu yake kavu isiyokuwa na ladha mbali na wewe, kwa kitendo chako hiki unalipa ruhusa tunda ya kuzipitisha Jeni zake, wakati ambapo limekupatia ladha tamu likiwa limeficha Jeni zake -ambazo ndio asili ya uhai wake- ndani ya moyo wa mbegu kavu iliyo kauka isiyo kupendeza, na pindi tu unapoitupa juu ya Ardhi huanza kuchipua wakati hali ya hewa

inaporuhusu kuanza kutengeneza mti wa matunda, ukiwa pamoja na matawi na majani na mizizi, Je, yote haya yanayotokea katika mimea hayamaanishi chochote!?.

L- Hivi ni nani aliyedhibiti malighafi za tunda hilo bubu lisiloongea, na akadhibiti kiwango cha sukari ndani yake kinachokuvutia?

Kisha: Ni nani aliyeifanya mbegu isipendeke na isilike, mpaka ufikie kuipuuza na kuitupa mbali!?

Kisha: Ni nani aliye ijaza malighafi za kutosha kuzaliana mbegu, na kwa ajili ya kutosha kuzalisha mmea mpya kwa aina zote za sifa yake na kazi zake?!.

m- Tumebaini hivi karibuni kuwa: hali (Inertia) tunayoishi ndani ya neema zake ni matokeo ya ganda la ulimwengu kwa ujumla.

Nini maana ya Inertia?

Chukua mfano: Ukipanda gari mara ghafla gari ikasimama, nini kinatokea?

Utasukumwa kwenda mbele! Si ndivyo?

Hii ndio maana ya inertia (Mshituko).

Laiti ingelikuwa Inertia katika ulimwengu wetu ni chache zaidi kuliko ilivyo hivi sasa basi punje ndogo ya upepo ingeweza kuitikisa Miamba, na katika ulimwengu hivyo hivyo tungekuwa tukikumbwa na matetemeko endelevu na ingezama kila aina ya vitu!.

Na laiti kama Inertia ingekuwa kubwa kuliko ilivyo hivi sasa basi tusingeweza hata kutikisa vidole vyetu.[2].

Na nguvu ya inertia hukaa katika (Mass) msongamano.

Na jambo lililo washangaza wanafizikia (Wanasayansi) nikuwa masi (mkusanyiko) ni njia ya utando, njia ambayo imekusanya kundi letu la mionzi ya jua, haihusiki katika kudhibiti inesha ila kwa kiwango cha 0.1% katika milioni moja, wakati ambao masi (Inesha) ya Ardhi haidhibiti inesha ila kwa kiwango cha 0.001% katika miliono moja.

Inesha au masi iliyopo ambayo tunapata uhai kupitia matokeo yake, na ambayo kupitia hiyo tunaweza kufanya harakati zetu, nayo ni matokeo ya mkusanyiko wa nishati za ulimwengu kwa ujumla.

"Hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yake kwa upuuzi na mchezo. Hiyo ndiyo dhana ya waliokufuru. Basi ole wao walio kufuru kwa Moto wa Siku ya Kiyama". [Surat Swad: 27]

Na elimu kila inapopanuka yanadhihiri maajabu na hekima na undani wa uumbaji![3]

n- Kisha nini kitafuata kama tutageuka kulitazama jicho:

Hiyo ni neema isiyopimwa kwa thamani yoyote duniani. "Hivi, hatukumuwekea macho mawili" [Suratul Balad: 8]

Nguvu ya ndani ya jicho ni sawa megapixels (ukubwa wa mega) mia tano na Sabini na sita.

Na jicho lina miliki lenzi safi mno kuliko zote Duniani.

Na saizi ya kipokea mwanga (Photoreceptor) katika retina hakizidi ukubwa wake nusu milimita za mraba, lakini kina uwezo wa kutofautisha kati ya mamilioni ya rangi pamoja na kuwa mbali, hii ni chalenji (Changamoto) na uumbaji wa kiuungu wa ajabu mno.

Unapo tazama kitu chochote mbele yako na mwanga ukaangukia katika retina ya jicho, basi katika hali hii hutokea mambo mengi ya kikemikali yaliyo ambatana na hilo, ambayo huzalisha mwisho wa tukio mkondo wa umeme (Electrical current), na huama mkondo huu kutoka katika retina ya jicho lako kupitia waya za neva (Nerve wires) kwenda katika ubongo, na ubongo hufanya kazi ya kutafsiri kutembea kwa mkondo huu wa umeme kuwa ndio kuona, hii ni kama kwamba ubongo una miliki kamusi kamili tangu zamani inayobadilisha mkondo huu wa umeme (Electrical current) ulio ufikia kuwa ndio kuona kwa kile kilichoko mbele yako.

Hili ni jambo la ajabu lenye kutisha sana ikiwa mtalifikiria!

Vuta picha: Ubongo huu umejificha ndani ya sanduku la mifupa lenye giza ambalo ni fuvu.

Na hakuna kinacho penya kuingia katika ubongo wako isipokuwa mikondo ya umeme (Electrical current).

Hivi ni jinsi gani ubongo unaweza kutafsiri huu mkondo wa umeme na kuwa ni kuona?

Ni jinsi gani unaweza kukupa kuona?

Chalenji (Changamoto) hii inatokea ndani mpepeso mmoja, kwa kitendo cha kufumbua macho yako na kutazama!.

Na swala hilo hilo upande wa macho:

Kiasi ambacho huingia mawimbi ya sauti ndani ya ngoma ya sikio lako, kisha ngoma ya sikio inayabadilisha kutoka katika mawimbi na kuwa harakati za mitambo (Michanical movement), kisha

---

[2] Tazama kitabu: Nature's Destiny: How the Laws of Biology Reveal Purpose in the Universe, Michael Denton.

[3] Ameyafafanua mambo haya Michael Danton katika kitabu chake kiitwacho: Nature's destiny, (Nguvu ya asili), na kitabu kimefasiriwa katika matoleo ya taasisi ya Darul Kaatib.

inahamisha harakati hizi za mitambo kupitia njia nyembamba sana zilizoko ndani ya sikio la kati na kuingia ndani ya sikio la ndani, ambalo huigeuza na kuwa mkondo wa umeme.
Mkondo huu wa umeme sasa hivi utahama kutoka katika sikio la ndani na kwenda katika ubongo, tayari ubongo unaanza kazi ya kuchambua mkondo huu wa umeme nakuwa sauti, na hapo tayari unasikia!.
Yote haya yanafanyika pia ndani ya kipindi cha chini ya sekunde moja: "Na Mwenyezi Mungu ndiye amekutoeni kutoka katika matumbo ya mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na akakuwekeeni masikio na macho, na nyoyo, ili mpate kushukuru" [Suratun nahl: 78]
Vuta picha kuwa ubongo unafikiwa na maelefu ya ishara za umeme (Electrical signals) kwa wakati mmoja kutoka katika jicho na sikio na ngozi, na kuonja, na kunusa, na kutoka katika viungo vingine tofauti tofauti vya mwili ili uweze kutofautisha kati ya ishara zote hizi kwa umakini, hili ni katika maajabu makubwa kuwahi kutokea. "Na vyote mnavyovishuhudia ni viumbe vya Mwenyezi Mungu, basi nioneshenі, enyi washirikina, imeumba nini hiyo miungu yenu mnayoiabudu badala ya Mwenyezi Mungu? Bali washirikina wameenda kando na haki na msimamo wa sawa waziwazi". [Suratu Luqman: 11] "Huo ndio ufundi wa Mwenyezi Mungu aliyetengeneza kila kitu vilivyo , hakika yeye anazo habari za yote myatendayo" [Suratun Namli: 88]
Hivi ni nani huyo awezaye kuihesabu na akaidhibiti neema moja miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu?
Hebu fikiria katika kila kiungo katika viungo vya mwili wako na katika kila mfupa unaokuwezesha kufanya harakati zako kwa thamani yake!
Fikiria viungo vyako laini ambavyo vinakupa uwezo wa kuvitikisa bila kugongana kati ya mifupa, wala kubanana, viungo hivi alivyo viwekea Mwenyezi Mungu ndani yake vitu kama mafuta ambayo huwekwa katika maungio ya vyombo mbali mbali vya kiufundi (Kama gani, katapila,kutiwa oil, grisi, n.k)
Fikiria katika neema za Mwenyezi Mungu kwa kuzingatia kushukuru neema zake aliye takasika.
NEEMA ZA MWENYEZI MUNGU HAZIHESABIKI "Kwani hamuoni, enyi watu, kuwa Mwenyezi Mungu amewadhalilishia vilivyoko mbinguni miongoni mwa Jua, Mwezi, Mawingu na vinginevyo, na vilivyoko ardhini miongoni mwa Wanyama, Miti, Maji na vinginevyo visivyodhibitika, na Akaeneza kwenu neema Zake za nje juu ya miili na viungo, na za ndani, kwenye akili na nyoyo, na zile Alizowawekea katika zile msizozijua? Na miongoni mwa watu kuna anayefanya ushindani juu ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtakasia ibada bila ya hoja wala ubainifu wala kitabu chenye kubainisha kinachofafanua uhakika wa madai yake". Suratu Luqman: 22

# 8- Baadhi wa pagani hupinga ushahidi wa kutiliwa manani na kusema kuwa kuna baadhi ya vitu si ukamilifu, mfano: Kama maradhi, na matetemeko?

Jawabu: Kutopatikana vitu vilivyo fanyiwa ufanisi katika ulimwengu kwa kiwango cha kufikia wapagani kuvizungumza hili halizuii uwepo wa ufanisi.
Kwa kitendo hicho vitu hivyo vinatia mkazo juu ya uwepo wa ufanisi katika ulimwengu.
Tuchukulie kuwa kusingekuwa na ufanisi kabisa, inamaanisha kuwa mpagani asingeweza kuyajua mambo yasiyo na ufanisi.
Swali la msingi: Unaanza kuzungumzia miundo ya vitu katika ulimwengu usiyokuwa na miundo?
Turudi: Ama vitu wanavyo vieleza kuwa havina ufanisi, haya ni mapungufu yao ya kielimu, au ni mapungufu ya kutozijua hekima za mambo hayo.
Waumini hawasemi kuwa ulimwengu umewekwa kila kitu kwa ufanisi kiasi kwamba hakuna matatizo, bali husema kuwa: Ulimwengu umeumbwa kwa ufanisi na hakuna kitu kinachotokea pasina sababu au malengo.
Msimamo huu wa mpagani, unafanana na mtu anaye pinga ufanisi wa vyombo vya anga kama ndege, ati kwa sababu ndani yake kuna kiwango kikubwa cha nishati ya mafuta ya petroli ambayo yanaweza kulipua usafiri huo wakati wowote![4]
Na ulimwengu haukutengenezwa ili uwe ulimwengu wa milele endelevu, na sisi hatukutengenezwa ili tuwe miungu!
Bali sisi tumetengenezwa ili tupewe mitihani kupitia kheri na shari. "Na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri, na kwetu sisi mtarejeshwa" [Suratul Anbiyaa: 35]

[4] Tazama kitabu: Dhwaahiratu naqdi ddini fil falsafatil hadiitha, cha Dr. Sultan Al Omariy, ikiwa ni risala yake ya shahada ya Udaktari.

Kheri na Shari na kila mitihani vyote hivi vinazunguka ndani ya mzunguko wa hekima na matashi ya kiuungu.

## 9- Ni kipi kinachozuia kuwa ulimwengu ulipatikana kwa sababu nyingine yenye kushikika au kuonekana; Mfano: Kama ustaarabu mwingine au kitu kingine chochote? Kwa nini awe ni Mungu wa tangu pekee?.

Jawabu: Kuna kanuni waliyoiweka wanachuoni wa kiislamu tangu takriban zaidi ya miaka elfu moja eliyopita , na kanuni hiyo inasema: "Mlolongo wa wafanyaji hupelekea moja moja kutofanyika kwa vitendo"[5]

Mlolongo wa wafanyaji: Yaani: Kupatikana kwa waumbaji wengi, na katika swali hili tuna utamaduni mwingine, na utamaduni ulio utangulia ndio uliozalisha huu, na huu utamaduni ulio watangulia ndio uliowazalisha hivyo hivyo na kuendelea, huu ndio mlolongo wa wafanyaji.

Na mlolongo huu hupelekea kwa akili ya kawaida katika kutokutokea kwa vitendo.

Kutokutokea kwa vitendo, Yaani: Kutokuwepo kwa viumbe mfano wa ulimwengu na binadamu na vinginevyo.

Kuwa na mlolongo kwa watendaji kunapelekea kutokupatikana kwa ulimwengu na uwepo wake.

Ikitokea moja ya utaratibu mmoja kusimama kutokutokea kwa utaratibu unaofuata, na unaofuata pia ukasimama usitokee kwa ule uliopita, na kuendelea mpaka mwisho, kamwe hautodhihiri ustaarabu huu wala ule uliopita wala unaofuata, wala isingedhihiri dunia wala kitu chochote.

Kwa sababu kila utamaduni utaishia pale ulipoishia uliokuwa kabla yake, na hapo hautodhihiri utamaduni wowote, na wala hakitodhihiri kitu chochote.

Hivyo ni lazima kuwe na muumbaji wa mwanzo na wa tangu, aliye kifanya kila kitu kuwepo.

Ikiwa mlolongo usiokuwa na mwisho, na kila mzunguko ulioko katika cheni unategemea ule ulio kabla yake, basi hapo hawawezi kupatikana viumbe wala kuumbwa wala chochote, kwa sababu mtendaji atasimama uwepo wake kwa mfanyaji alie mtangulia, na huyo aliye tangulia atasimama kwa kusimama aliye kuwa kabla yake na kuendelea, na kitakachofuata ni kutokupatikana kitu chochote.

Na ni lazima cheni itasimama kwenye kikomo.

Na hapa lazima tukubaliane kuwa kuna muumbaji wa mwanzo ambaye hakimtangulii kitu chochote!.

## 10- Sisi twazifahamu kanuni zinazo uendesha ulimwengu, na tunazijua sababu za matetemeko ya ardhi vizuri, kwa nini tuhitaji muumbaji wakati tushazijua kanuni?

Jawabu: Anapiga taswira mpagani kuwa kanuni zinatosha kuumba ulimwengu na kutokea kwake, na baadhi ya wapagani wanategemea mtazamo wa: "Nguvu ya mvutano" (Gravitation force), na kuwa inatosha kuufanya ulimwengu uwepo, na baadhi ya mitazamo ya kuubatilisha mtazamo huu moja kwa moja ni kitendo cha kufikiria chanzo cha mtazamo huu wa nguvu ya mvutano, au ni nani aliye tunga kanuni hii, au ni nani aliyempa sifa ya kuingia na kuonyesha athari ziliko ndani yake?.

Kwa kufumbia macho vitu hivi ambavyo vinajulikana bila ya kusoma, nikuwa kanuni au mtazamo wa Nguvu ya mvutano, haisababishi kubingirita kwa mpira wa mchezo wa biliadi (pool)!.

Hivyo, Nguvu peke yake haiwezi kufanya kitu chochote pasi na kudhihiri kitu.

Hivyo, Nguvu ya mvutano (Gravitation force) haiwezi kuzalisha kimpira cha biliadi bali inaweza kukitikisha pekee itakapopatikana nguvu hivyo na kikapigwa kwa fimbo ya biliadi (Pool).

Nguvu ya mvutano si kitu kinachojitegemea bali ni wasifu wa tukio la asili (Kawaida).

Na nguvu ya mvutano kamwe haitoweza kutikisa kimpira cha biliadi bila kupatikana nguvu ya msukumo au kuikandamiza fimbo ya biliadi (Mchazo wa puli) na hapo itakitikisa na hapa ndipo kitaweza kutikisika kimpira hicho na kuonekana nguvu ya mvutano.

Lakini mpagani analeta taswira ya kuwa kupatikana kwa nguvu ya mvutano (Gravitation force) kuna tosha kutengeneza kimpira cha biliadi na fimbo yake, na kukizungusha kimpira hicho! (Haingii akilini!).

Ni kipi kilicho karibu zaidi kati ya akili na mantiki katika sababu za kutokea hii dunia:Ni muumbaji au mvutano?

---

[5] Tazama kitabu: Dhwaahiratu naqdi ddini fil falsafatil hadiitha, cha Dr. Sultan Al Omariy, ikiwa ni risala yake ya shahada ya Udaktari.

Na tupige mfano mwingine: Mfumo wa moto unaozalishwa ndani ya mota ya gari hauwezi kutengeneza mota nyingine.
Na ikiwa tutauongezea mfumo huu moto mwingine ndani ya mota ya gari, basi mota haitoweza kufanya kazi, ni lazima kuwe na mafuta yanayozalisha nishati, na lazima kuwe na cheche zinazozalishwa, na ni lazima kabla ya hapo pia kuwe na mota, na hapa pekee ndipo utakapopatikana mfumo wa moto na kufanya mota ifanye kazi!.
Haingii akilini kuleta taswira na kufikiria kuwa mfumo wa moto ulioko ndani ya mota unatosha kuitengeneza mota na cheche zinazozalisha moto na kutengeneza mafuta na kumtengeneza dereva pamoja barabara.
Mtazamo wa kutosheka na nguvu ya mvutano (Gravitation force) kwa kuutafsiri uwepo wa ulimwengu ni fikra isiyoingia akilini hata kidogo.
Kisha fikra hii ikiwa tutaichukulia kuwa inawezekana, basi itatupeleka kuwa na mtiririko wa watendaji ambao tumetoka kuuleza katika jibu la swali lililo tangulia,ni nani aliyetengeneza nguvu hiyo ya mvutano,na ni nani aliye mleta yeye?, na ikiwa watadai kuwa ni nguvu nyingine,hapo tutaingia katika mtiririko wa watendaji ambao mwisho wake utaishia kutokuwepo kwa nguvu yoyote,au kiumbe chochote.

## 11- Ni kipi kinazuia kuwa chanzo cha dunia ni ghafla (kama ajali)?.

Jawabu: Kauli ya kusema: Ulimwengu ulitokea ghafla,ni kutojua misingi ya maswali ya uwezekano; Kwa sababu jambo la ghafla lina sharti mbili zisizotengana.
Ambazo: Ni wakati na mahali.
Jambo la ghafla ni sharti ndani kuwa na muda ambao tukio hilo lilileta athari zake.
Na ni sharti pia kuwe na malighafi mahali ambazo zitaleta matokeo ya kitendo kilicho kusudiwa.
Inawezekanaje tuamini kuwa ghafla imeuleta ulimwengu hali yakuwa imetokea bila muda wala sehemu!?.
Inawezekanaje kutokea ghafla bila ya hiyo ghafla kuweko mwanzo?
Ni vipi ghafla inaweza kuleta athari kabla ya kuwepo kwake na kuwepo wakati wa kutokea kwake na mahali pa kutokea,ambavyo ndiyo sharti la msingi la kutokea kwa tukio lolote?.

## 12- Vipi tunaweza kumjibu mpagani anayesema kuwa ulimwengu ni wa tangu?.

Jawabu: Kulingana na kanuni ya pili ya Thermodynamic (Second law of Themodynamic) ya kupima kiwango cha joto inaonyesha kuwa haiwezekani dunia kuwa ya tangu isiyo na mwanzo.
Kwa upana zaidi tunakupa mfano huu kwa ufafanuzi zaidi: Ikiwa utakuwa na kikombe cha maji ya moto chumbani, basi joto la maji litahama kutoka katika maji ya moto mpaka ndani ya chumba mpaka joto la chumba lilingane na joto la maji ya kikombe, hii ndio maana ya kanuni ya pili ya joto ya Thermodynamic, kiasi kwamba joto linatembea kutoka juu mpaka chini wakati wote.
Na kanuni hii inatokea katika kila kitu katika ulimwengu tena kila wakati tangu kutokea kwa ulimwengu, mpaka joto la kila kitu linalingana sawa katika dunia, na ikitokea joto kuwa na kiwango sawa katika kila kitu duniani, basi hapo kitatokea kitu kinachoitwa kuharibika ama kufa kwa joto katika ulimwengu (Thermal Death of Universe).Na laiti kama ulimwengu ungelikuwa ni wa tangu (Yaani hauna mwanzo) basi ilitakiwa sasa hivi uwe umesimama (Kiwango cha joto kimetoweka), lakini uhalisia kwa sasa ni kuwa ulimwengu uko katika hali ya chini ya entropy, na bado haujafika katika kiwango cha kutoweka ama kufa kwa joto, hivyo jawabu nikuwa ulimwengu si wa tangu, bali una mwanzo wa uhakika ambao ulitokea ukiwa pamoja na wakati na mahali pia.
Na unaweza kutokea pia kulingana na kanuni hiyo hiyo kuwa ulimwengu ulianza katika kiwango cha chini cha entropy, na hii inamaanisha kuwa kutokea kwake hakukuwa na mfano kabla yake -Umeanzishwa-.
Hii ni kanuni ya kisayansi kwa upande mwingine, lakini wakati huo huo upagani uko upande mwingine kabisa.

## 13- Ni kwanini haizingatiwi kanuni ya sasabu kwa muumbaji? Au kwa maelezo mengine: Ni nani aliyemuumba muumbaji?

Jawabu: Kwanza: Muumbaji hazimuhusu kanuni zote za viumbe wake na swala hili halihitaji kusoma.
Na vinginevyo itatupidi tuseme: Ni nani aliyepika kupika?
Na ni nani aliyempaka rangi mpaka rangi?
Muumbaji anajulikana hata bila kusoma kuwa yupo tangu zamani na ana mahali, hivyo haziendani naye kanuni zote, kwani yeye ndiye alizifanya ziwepo -Huyu Mtakasifu-

Pili: Kila chenye kuzuka ni lazima kiwe na mletaji,na hili liko sahihi (Kila mtu anakubali hilo), lakini muumbaji "Hakuna chochote mfano wake" Suratu shuura: 11.
Tatu: Muumbaji hakuzuka (bali ni wa tangu na tangu) Hivyo, tunaweza kusema kuwa ni nani aliyemuumba?.
Nne: Ni lazima muumbaji awe wa tangu na tangu wa lazima kuwepo,na tukilikataa hili itatulazimu kuingia katika tatizo la "Mlolongo wa watendaji,ambao moja kwa moja unapelekea katika kutokuwepo mtendaji" na hili tumekwisha lieleza hapo awali kwa upana, ni lazima muumbaji awe wa lazima kuwepo kwake wa mwanzo asiye na mwanzo -Mtakasifu-.

# 14- Ulimwengu ni mkubwa; Inawezekanaje kwa miili yetu hii midogo tuwe kituo cha ulimwengu huu mpana kiasi hiki?

Jawabu: Mpagani huleta taswira zisizo na msingi, na kusema kuwa: Kwakuwa ulimwengu ni mpana, hivyo mwanadamu si kituo cha ulimwengu huu!.
Mtazamo huu: Umejengeka katika jambo jingine nyuma yake, nalo nikuwa: Shamba pana na mmiliki wake umbile lake ni dogo sana ukilinganisha na shamba: Hii inaonyesha kuwa shamba si lake!.
Kinachozingatiwa si umbile tu.
Na tabia ambazo hazina umbile la kushikika ndio kipimo kikubwa cha kuzidiana katika mtu mkubwa na dhalili.
Watu hupimwa kwa tabia zao.
Swala la maumbo si kipimo!
Hebu wacha tupige mfano huu: Tuchukulie kuwa laiti tungelikuwa na mfalme, na mfalme huyu akawausia watoto wake baadhi ya usia na nasaha, na akawaandikia maandishi, hivi inawezekana kuja mpinzani akasema: Inawezekanaje Mfalme anayemiliki maelfu ya hekari ya Ardhi tena makubwa yasiyohesabika, akae anashughulika na mwanaye ambaye umbile lake halifikii sehemu moja katika mamilioni anayoyamiliki Mfalme huyu katika Ardhi na mahekari?
Na Mwenyezi Mungu anamfano wa juu zaidi kuliko huu.
Hivi kiukweli upinzani huu unaingia akilini?
Hoja si maumbile wala uzani.
Kisha, kwani huu si ndio ulimwengu ulioanza kwa tone dogo kuliko kichwa cha rungu, kwa mabilioni ya mara, kama anavyolikubali hili kila mwanafizikia wa dunia?
Hivyo umbile ni swala la kunasibishwa tu.
Kisha, ni kipi kinachomdhuru mpingaji (Mpagani) ikiwa Mwenyezi Mungu ataumba akitakacho kwa namna aitakayo?
Je, Mwenyezi Mungu anapata tabu katika kupata malighafi, mpaka afikie kutoa kulingana na mahitaji pekee?
Ametakasika Mwenyezi Mungu kuwa na jambo hilo.
Lakini, hivi ni kweli sisi tunaukamilifu kabisa wa kuishi katika ulimwengu huu?
Naam, ndiyo, ewe mwanadamu: Tunakuwa na makazi katika ulimwengu huu kwa mujibu wa sheria za Mwenyezi Mungu.
Maana ya sheria ya Mwenyezi Mungu ni: Dini.
Dini ni amana uliyoibeba, nao ni Mtihani mkubwa ambao unajukumu la kuutekeleza.
Hivyo wewe mwanadamu unatakiwa kuwa mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa hili unakuwa wewe ndio mkazi wa ulimwengu huu, wewe ndiye mkazi na kitovu cha ulimwengu huu, si kwa sababu ya umbo lako wala nguvu zako wala kwa uwezo wako bali ni kwa sababu ya sheria(kazi) ya Mwenyezi Mungu.
Na wewe unauwezo wa kufanya mazuri na kuacha shari, unauwezo kufuata imani na ukafiri.
Kila mmoja wetu anajua kuwa yeye anaulazima wa kubeba majukumu (Mkalafu), sawa sawa tumetaka au tumekataa!
Mpingaji na muumini na mpagani kila mmoja anafahamu kuwa yeye ni mukalafu (anawajibika kubeba majukumu) na anahisi kuwa anajukumu la kufanya katika sheria za Mwenyezi Mungu, na anasumbuliwa na tatizo kuchomwa na nafsi yake (Wasi wasi), litokanayo na maadili, na anajua ndani ya moyo wake kuwa kuna kitu: Fanya na usifanye. Fanya mazuri na usifanye shari, kila mmoja wetu anajua kwa uhalisia kabisa kuwa anawajibu wa kufanya!.
Hivyo, sisi tuko katika Makazi ya ulimwengu huu kwa ajili ya kubeba wajibu (Majukumu).
Na pia tupo katika Makazi ya ulimwengu huu kwa hisia na akili zetu, tunajua na tunaelewa na kufahamu ukweli wa kuwepo kwetu (wala si ndoto), na uhalisia wa ulimwengu unaotuzunguka, na tunafahamu vizuri maana ya kuwepo kwetu.

Hivyo, sisi ndio waamrishwaji, wenye kulipwa ama kuadhibiwa, tuliobebeshwa jukumu, na wenye kuhesabiwa, na si mwingine!

Na sisi ndio viumbe pekee tunaoelewa ufanisi wa ufundi katika kushughulikiwa mambo yetu, sisi ni viumbe tunaoelewa vizuri ufanisi huo, sisi ni viumbe tunaoweza kuyatekeleza tuliyowajibishiwa, au kuyakataa maamrisho hayo, sisi tunauweza wa kutosha kuwa na maamuzi, sisi tunauwezo wa kuamini na kukufuru.

Hivyo, sisi tuko katika Makazi ya huu ulimwengu. "Hakika sisi tulidhihirisha na kizweka wazi amana-ambayo Mwenyezi Mungu amewapatia waliokalifishwa sheria waitunze, nayo ni kufuata maamrisho na kujiepusha na makatazo- kwa mbingu, ardhi na majabali, vikakataa kuibeba na vikaogopa visiweze kusimama kuitekeleza, na akaibeba binadamu na akashikamana nayo pamoja na udhaifu wake. Hakika yeye ni mwingi wa udhalimu na ujinga wa nafsi yake". Suratul Ahzab: 72

# 15- Wanasema baadhi ya wapagani: Ziko sayari nyingi sana, na hivyo, kwa mujibu wa nadharia ya "Uwezekano wa asili" yawezekana kukawa na Sayari katika Sayari hizo inayowezekana watu kuishi ndani yake. Je, ni sahihi kuleta ushahidi huu?

Jawabu: Kuna mahusiano gani kati ya kuwepo kwa Sayari nyingi na kupinga dalili ya ufanisi?

Swala si malighafi za awali.

Kuwa kwangu katika msitu wa kijani wenye kila aina ya matunda na wanyama, haimaanishi ndio kijitokeze mbele yangu chombo ghafla chenye chakula kilichopikwa na chenye ladha; Hivyo, kumbe suluhisho si kuwepo kwa malighafi tangu mwanzo!

Pia kuwepo kwa makaa ya mawe katika majangwa ya ulimwengu, haimaanishi kuwa ndio naweza kupata mfumo wa usindikaji wa digitali (Digital processors) na mfumo wa umeme ambao hutengenezwa kutokana na makaa ya mawe, ambayo yananizunguka kila mahali katika jangwa!

Hivyo, suluhisho si kuwepo kwa Malighafi tangu awali; Kumbe kilichopo hapa ni utengenezaji na ufanisi, na kujua ilifanyika vipi?

Kitendo cha kuwepo kwa idadi kubwa ya Sayari hakitoshi kutokea Sayari kati ya hizo iliyotengenezwa kwa ufanisi mkubwa kama Ardhi.

Alaah!, kumbe la msingi hapa ni ufanisi na uumbaji na utengenezaji. "Huo ndio Ufundi wa Mwenyezi Mungu aliyetengeneza vilivyo kila kitu" [Suratun Namli: 88]

Kuwepo kwa Sayari zingine nyingi hakutoi jibu la moja kwa moja la kuwepo kwa maisha juu ya Sayari ya Ardhi.

Kuwepo kwa Sayari nyingi hakutoi majibu sahihi ya mfumo wa kurithiana kwa vinasaba vilio ndani yako wenye takribani kazi bilioni nne unaodhibiti kila shughuli zako na viungo vyako na homoni zako kwa udhibiti wa hali ya juu, kabla hata hujazaliwa wewe!.

Hivyo, maisha yanafahamika na wala si kiini, kisichofahamika.

Ikiwa tutapanda mimi na mpagani mmoja juu ya Sayari moja miongoni mwa Sayari na tukagundua kifaa kilichofungwa na kinafanya kazi ya kudhibiti mfumo wake kwa ufanisi, hata kama tutakuwa hatujafahamu kazi yake, je, inawezekana kupinga kuwa hakuna aliyekitengeneza kifaa hiki, ati kwa kwa sababu tu ya ukubwa wa Sayari tuliyomo ndani yake?

Akili ya kawaida inatusukuma mimi na mpagani wakati tunapoona kifaa hiki kusema kuwa "Ama kweli aliyekitengeza anauwezo mkubwa".

Na anayepinga jambo hili lisilohitaji kusoma, yaani anayepinga kuwepo kwa aliyekiweka, huyu ndiye anayetakiwa kuleta ushahidi, na siyo aliyethibitsha kuwepo!.

Mpingaji katika ulimwengu huu mzuri na uliopangika ndiye anayetakiwa kuleta ushihidi, na siyo Muumini ndiyo mwenye kutakiwa kuleta ushahidi!

Kuna wakati aliandika mpagani asiyefkubali uwepo wa Mungu Carl sagan riwaya kwa jina la: "Mawasiliano" (Contact), akieleza ndani yake ni jinsi gani wanasayansi wanatafuta ubunifu nje ya Ardhi.

Na katika riwaya ya kubuni wamegundua wanasayansi mlolongo mrefu wa namba za mwanzo zinazokuja kutoka anga la nje; Na hii ni kwa sababu mlolongo huu wa mwanzo unaleta maana ya kiwango maalumu cha hesabu, kiwango kinachoonyesha aina fulani ya matengenezo, huu ukawa ni ushahidi wa kiakili wenye kujitosheleza kutoa jibu la uhakika kuwa ujumbe huu umekuja kutoka katika utamaduni mwingine unaojaribu kuwa na mawasiliano nasi!.

Chaajabu: Nikuwa Bw. Carl Sagan asiyekubali uwepo wa Mungu(Agnostic), ni mtu maarufu, lakini akili yake inakubali ukweli wa itikadi na mfumo katika ujumbe mfupi uliotangulia kuwa ndio ushahidi wa kupatikana kwa ulimwengu na kuimarishwa kwake!.

Kwa mlolongo tu wa namba za mwanzo unaweza kukubali kwa uhakika uwepo wa maisha ya wazi; Unawezaje kunasibisha bilioni nne ya kazi zilizoko ndani ya kila seli miongoni mwa seli za mwili wako, ambazo ikiwa itaharibika kazi moja miongoni mwazo litatokea janga, unawezaji kunasibisha ufanisi wote huu katika uongo wa kipagani usio na Hoja sahihi.

Haingii akilini hata kidogo, kuhukumu kupitia uongo ili kukataa tafsiri ya wazi iliyoko dunia nzima juu ya muumbaji. "Sema, ewe Mtume, kuwaambia watu wako, «Fikirini na mzingatie kwa yaliyomo mbinguni na ardhini miongoni mwa aya za Mwenyezi Mungu zilizo waziwazi.» Lakini aya, mazingatio na Mitume wenye kuwaonya waja wa Mwenyezi Mungu adhabu Yake, vyote hivyo havikuwa ni vyenye kuwanufaisha watu wasioamini chochote katika hivyo, kwa sababu ya kupa mgongo kwao na ujeuri wao". Surat Yasin.

## 16- Kwa nini kusiwe na muumbaji zaidi ya mmoja wa tangu?

Jawabu: Amesema Allah Mtukufu: ""Lau mbinguni na ardhini kungekuwa na waungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu, kutakata na sifa za upungufu ni Kwake na kutukuka ni Kwake, wenye kuyaendesha mambo yake, ungaliharibika mpango wake". Suratul Anbiyaa: 25

Kuwepo kwa Mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu kunapelekea kuwa na miungu wengi, na wingi wa miungu unapelekea uhitaji.

Na uhitaji kwa muumbaji -Haiwezekani kwake Mtukufu- unapelekea kutoweka kwa amani katika ulimwengu na kuwa unaweza kuporomoka. Na hii inapelekea kuharibika kwa ulimwengu.

Hakuna dhamana ya kubaki kwa ulimwengu ukiwa na Mungu muhitaji!.

"Lau mbinguni na ardhini kungekuwa na waungu wasiokuwa Mwenyezi Mungu, kutakata na sifa za upungufu ni Kwake na kutukuka ni Kwake, wenye kuyaendesha mambo yake, ungaliharibika mpango wake. Basi Mwenyezi Mungu, Bwana wa 'Arshi, Ameepukakana na sifa za upungufu na ametakasika na kila sifa ambayo wakanushaji makafiri wanamsifu nayo ya uongo, uzushi na kila aibu". Suratul Anbiyaa: 22

Ametakasika muumbaji na kuhitaji na kuwa na haja, Yeye ni Mkwasi Msimamizi Aliyetakasika.

Ongeza juu ya hayo yaliyotangulia: Kuwa laiti kungelikuwa na miungu wawili au zaidi, uwezekano wa kupingana ni jambo linalotarajiwa zaidi katika akili kuliko kukubaliana, kwa sababu uwepo wa miungu wengi unamaanisha uwepo wa matashi mengi, na maamuzi mengi, na kuwepo kwa maamuzi mengi kunamaanisha uhitaji wa kila mmoja, na hii inapelekea kuharibika kwa mbingu na ardhi.

Na maumbile ya mwanadamu yanakiri kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja, na laiti angetazama mwanafizikia au yeyote katika ulimwengu huu hatopata picha kamili zaidi ya kuwa na muumbaji mmoja, haya ndiyo maumbile.

## 17- Kwanini Dini?

Jawabu: Mpagani mkorofi zaidi huamini kuwa ukweli ni bora kuliko uongo, je, sivyo hivyo?

Mpagani mkorofi zaidi anaamini kuwa uaminifu ni bora kuliko hiyana, je, sivyo hivyo?

Misemo hii haiko katika ulimwengu huu, na hakuna katika ulimwengu kinachothibitisha maana yake wala makusudio yake.

Nini maana ya ukweli?

Nini maana ya uaminifu?

Je, ikiwa tutafumua ndani ya punje ndogo tunaweza kupata maana mfano wa ukweli au uongo?

Ikiwa tutapata nishati ya kiumbe kikubwa zaidi au homoni ya kiumbe kidogo zaidi duniani, je, tunaweza kupata uhalisia wa amana au hiyana ndani yake?

Na msamiati huu hauko katika dunia hii tunayoiona.

Lakini ni msamiati wenye ukweli.

Bali ni katika mambo makubwa.

Thamani ya mwanadamu ni kwa tabia zake, na si kwa umbile lake hili, na wala si kwa idadi ya vimelea vyake, na wala si kwa kiwango cha seli alizonazo.

Thamani ya mwanadamu ni kwa kushikamana kwake na maamrisho ya Mwenyezi Mungu ndani yake.

Na thamani hii hakuna chochote kinachoweza kushirikiana na mwanadamu.

Kuna mtu mwema na mtu muovu.

Lakini hakuna mlima mwema na mlima muovu.

Na wala hatuwezi kupata Sayari yenye uaminifu na Sayari yenye hiyana.

Mwanadamu pekee ndiye aliyekusudiwa kuipata thamani hii ya hali ya juu na ndiye aliyetiliwa manani uwepo wake.

Mwanadamu na Jini pekee ndiyo viumbe wanaojitambua kuwa wanamajukumu.
Na si vinginevyo, hisia za kutambua maana ya maadili isipokuwa ni sehemu ya maumbile ya kutambua amri ya Mwenyezi Mungu, iliyoko ndani ya kila mmoja wetu.
Dini ndiyo jambo la dharura na la lazima kwa mwanadamu kulijua.
Dini ndiyo kitu pekee kinachoweza kuweka wazi maana ya maadili, na ni kwa nini yawepo, na ni kwa nini tunakuwa na hisia za kuhisi ni kwa nini ni muhimu maadili kuwepo.
Kitu pekee kinachoyapa maadili muonekano wake halisi ni dini.
Maadili haiwezekani kuyafahamu isipokuwa kwa mfumo wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu.
Na haiwezekani kutambua ni kwa nini jambo hili ni maumbile yaliyoko ndani ya mwili wa mwanadamu isipokuwa kwa kupitia dini.
Na kupitia dini ndio tunatambua lengo la kuwepo kwetu, na tunatambua maadili ambayo tunahisi kuwa tunaulazima wa kushikamana nayo, hata tusiposhikamana nayo, ni sehemu ya amri za Mola Mlezi.
Dini ni jambo la dharura na la lazima kibinadamu.
Na kupitia dini tunafahamu ni kwanini sisi leo tuko hapa?
Na tunafahamu ni kipi kitaendelea baada ya kifo?.
Na tunafahamu maana ya uwepo wetu.
Na tunatambua ni kipi kinatakiwa kwetu katika maisha haya?
Dini ndiyo jibu halisi la kutambua mambo muhimu yanayomshughulisha mwanadamu.
Na ndiyo maana ikikosekana dini ulimwengu mzima unageuka kuwa kipofu kamili usiyokuwa na maana kabisa.
Anasema bin Qayyim -Mwenyezi Mungu amrehemu-: "Hakuna njia ya furaha na kufanikiwa si duniani wala akhera isipokuwa kupitia mikononi mwa Mitume, na hakuna njia nyingine ya kujua kizuri na kibaya kwa ufafanuzi isipokuwa kupitia kwao, na hazipatikani radhi za Mwenyezi Mungu milele ila kupitia mikono yao"[6]
Dunia ni giza, tena imelaaniwa, isipokuwa kile kilichochomozewa na Jua la dini na jua la Utume, kama anavyosema Sheikhul Islami bin Taimiya -Mwenyezi Mungu amrehemu-[7]
Pasi na dini haliwezi kufahamika lengo halisi la maisha wala maana ya wema wala thamani yake.
Na bila utume ulimwengu hugeuka mchezo mbaya wenye kutisha
Dini inapotoweka na watu wakapinga utume kwa wakati huo huo, watu hugeuka na kuwa makapi ya Sayari kama asemavyo Carl Sagan, na kuwa wadudu kama asemavyo Sartre.[8]
"Na mwanadamu anakuwa ni kama makapi ya kemikali, au kwa maana ya ndani zaidi, ni kama uchafu wa kemikali (Chemical Scum) kama anavyosema Steven Hawking[9].
Utume ndio muhimili pekee wa maisha, na pasina kuwa na dini hugeuka ufundi mkubwa unaobuniwa na starehe nzuri kuwa hofu!
Bila dini hugeuka ulimwengu kwa uzuri wote ulionao kuwa ndoto za kutisha.
Hata wewe ukimuuliza mpingaji yeyote swali lolote la maisha, mfano: Ni kwa nini sisi tuko hapa ulimwenguni, au nini kinafuata baada ya kifo?
Basi, ni moja kati ya mambo mawili, ima aone swali lako halina mantiki, au ashikamane na majibu ya kukisia yasiyo na uhakika.
Hivyo, dini ndio muktadha pekee wa asili wa kumfahamu mwanadamu na kufahamu ulazima wa maadili na tabia njema, na ndio jambo la msingi la kufahamu maana ya maisha na lengo la maisha, na kuhakikisha kumuabudu Mwenyezi Mungu, ibada ambayo ndani yake kuna kuokoka.

## 18- Kipi kinazuia maadili na tabia hizi kuwa ni matokeo ya akili za watu au jamii fulani?

Jawabu: Ubongo umetengenezwa kwa malighafi zile zile ambazo zimetengeneza ulimwengu huu tunaouona!
Kwa vyovyote vile ubongo utakavyo shikamana au kutengenezwa kikamilifu hii ni sawa ni sifuri, sifuri hata zikiwa nyingi kiasi gani haziwezi kutoa majibu zaidi ya sifuri.

---

[6] Tazama kitabu: Zaadul Ma'ad: Juzuu ya 1 uk. 68.
[7] Tazama: Majmu'ul Fataawa: Juzuu ya 19, uk. 93-94.
[8] Video Source: The Shores of the Cosmic Ocean [Episode 1] Some part of our being knows this is where we came from. We long to return. And we can. Because the cosmos is also within us. We're made of star-stuff. We are a way for the cosmos to know itself. 06 min 04 sec. Ama mwanadamu kuwa kama wadudu amelieleza hili Sartre katika riwaya yake ya (Ghitiyani) Yaani: Taharuki, akisema:
[9] From an interview with Ken Campbell on Reality on the Rocks: Beyond Our Ken, 1995

Ikiwa malighafi haijui zuri wala baya, hata ubongo kadhalika!
Na hapa tunamuuliza mpingaji: Imewezaje kutokea maana ya mazuri na mabaya ikiwa ulimwengu mzima tunaoushuhudia umepinda kimaadili, haujui heri wala shari?
Na swali la pili: Ni kipi kizuizi cha akili cha kutowaangamiza viumbe wote wa Ardhini?
Na kipi kizuizi cha akili kinachofanya kutowaingiza binadamu wa kiwango cha chini katika mazizi ya wanyama?.
Ni kipi kizuizi cha akili kinachofanya kutowaua wagonjwa na walemavu na vikongwe na koo dhalili, kama ilivyotokea katika mradi wa uchaguzi wa asili, alioutekeleza Nazi, mradi wa maonyesho ya televisheni (Action Tv Project)[10]
Na maswali haya ubongo huu unaojulikana hauwezi kuyajibu kuwa ni sahihi au si sahihi.
Hivyo, ubongo utasimama bila shaka katika upande huu wa maadili, kwa sababu umetengenezwa kutokana na chembe hizo hizo za Ardhi.
Hivyo, hakuna mahusiano kati ya ubongo na maadili na kati ya tabia njema, si hapa wala pale.
Ama mtazamo wa kuwa jamii ndio chanzo cha maadili, huu ni mtazamo wa ajabu!, kwa sababu tabia kama tabia zinamuhusu mtu mwenyewe na si jamii kama jamii.
Kisha jamii hiyo hiyo imetokana na malighafi hizo hizo, hivyo, jumla kubwa ya masifuri kwa mara nyingine ukiijumlisha haiwezi kuleta jibu zaidi ya sifuri, je, jamii imezalisha vipi maadili, hali yakuwa maadili hayo hayahusiani na ulimwengu huu wenye kuonekana kabisa?
Kisha tuchukulie kuwa maneno haya yako sawa, na tukubali kuwa maadili chanzo chake ni jamii, hapa Nazi atakuwa yuko sawa katika kuwaua wenzake kwa sababu jamii nzima anaiyona hivyo.
Ulimwengu ulipokubaliana kumuhukumu Naaziy, maamuzi haya yalitolewa kulingana na fikra yakuwa maadili ni jambo huru, wala jamii si chanzo chake, tukilikataa hili maana yake wasingeweza kumuhukumu Naaziy, na wasingeweza kujua kuwa alifanya makosa tangu awali.
Hivyo, maadili ni kitu kinachojitegemea kando na jamii, haki ni haki tu sawa iwe mbele ya jamii njema au jamii mbovu.
Na kosa ni kosa tu, sawa liwe mbele ya jamii njema au jamii mbovu.
Hivyo maadili yanamaana yake ambayo iko juu ya ubongo wa jamii.

# 19- Kuna miungu wengi katika tamaduni mbali mbali za ulimwengu, ni kwa nini iwe imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu tu?

Jawabu: Hapatikani muabudiwa katika dini zote za ardhini isipokuwa Mwenyezi Mungu.
Na tofauti yetu na dini zingine zilizobakia nikuwa; Wao wamefanya miungu wengine wadogo wadogo kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu, mfano: Yesu, na Roho Mtakatifu, kwa wakristo, na mungu Fashno na Shifa na Barahima kwa wahindusi, n.k.
Hivyo, dini zote zinamuamini Mwenyezi Mungu mmoja wa pekee na kwao huyo ndiye muumbaji wa Ulimwengu.
Lakini wanaweka pamoja na Mwenyezi Mungu miungu wengine wengi.
Bali hata masanamu ya washirikina, hawakuwa wakiyafanya kuwa miungu yenyewe, bali walikuwa wakikiri kuwa Mwenyezi Mungu ndiye muumba, lakini walikuwa wakiyafanya kuwa ndio wawakilishi wao kwa Mwenyezi Mungu Na ukiwauliza, ewe Mtume, hao washirikina, »Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi kwa mpango huu mzuri na akalidhalilisha jua na mwezi?» Watasema, «Aliyeviumba hivyo ni Mwenyezi Mungu Peke Yake.» Basi vipi wao watapotoshwa waache kumuamini Mwenyezi Mungu, Muumba na Muendeshaji wa kila kitu, na wakawa wanamuabudu asiyekuwa Yeye? Basi uonee ajabu uzushi wao na uongo wao! Suratul Ankabut: 61
Anasema Sheikhul Islam bin Taimiya -Mwenyezi Mungu amrehemu-: "Na atakayewadhania waabudu masanamu kuwa walikuwa wakiamini kuwa yaliumba ulimwengu au yanashusha mvua au yanaotesha mimea au yanaumba wanyama au mengineyo, huyu atakuwa mjinga hawajui, bali lilikuwa lengo la waabudu masanamu kwa masanamu yao ni sawa na washirikina wanaoyatukuza makaburi"[11]
Na anakiri Will Durant kuwa asili ya uhindusi ni kuabudu masanamu ambako kunarudi asili yake katika kumuamini Mwenyezi Mungu mmoja na wa pekee, anasema kuhusu miungu ya Wahindusi: "Haya maelfu ya miungu ndicho wanachokifanya makanisa ya kikristo, katika kutukuza maelfu ya watakatifu, haingii

[10] https://en.wikipedia.org/wiki/Aktion_T4
[11] Majumuul Fatawa: Juzuu ya 1 uk. 359.

katika akili ya Muhindi hata kidogo kuwa maelfu miungu hii yasiyo na idadi ati yana utukufu wa hali ya juu"[12].
Na ilieleza ripoti iliyofikishwa katika serikali ya Uingereza India wakati wa uvamizi wa Uingereza India yakuwa: "Matokeo ya jumla ambayo yamefikiwa na jopo la utafiti nikuwa Wahindi wengi wanaitikadi ya kuamini Mungu mmoja aliye juu".[13]
Hivyo, Mungu ni mmoja katika dini zote za ardhini. "Na Mola wetu Mlezi ni Mola mmoja" Suratul Ankabut: 46 Na masanamu haya, na miungu hawa si chochote isipokuwa ni wawakilishi wa kumkufuru Mwenyezi Mungu "Na wale waliowafanya kinyume na Yeye kuwa ni vipenzi (Husema) Sisi hatuwaabudu, isipokuwa (tunataka) watuweke karibu zaidi na Mwenyezi Mungu" Suratul Zumar: 3

## 20- Ikiwa mtu atafanya jambo ambalo halihitaji basi huu ni mchezo! Na Mwenyezi Mungu hana haja na sisi, hivyo, ni kwa nini alituumba?

Jawabu: Mtazamo wa kusema kuwa haja huendana na mchezo, hii ni fikra ya kipumbavu!
Haja huendana na hekima (Lengo) wala si mchezo.
Daktari tajiri mwenye cheo kizuri anaweza kuwatibu watu bila ya kuwa na hitajio lolote kutoka kwao, bali anawatibu kwa ajili ya masilahi yao wao, na hapa hatuwezi kusema kuwa kitendo chake hiki ni mchezo usio na maana!
Hekima na makusudio makubwa yaliyoko nyuma ya kufanya hayazunguki katika kuhitaji au mchezo usio na faida!
Na mmoja kati ya waogeleaji anaweza kumuokoa mtoto kwa sababu ya kumuhurumia kisha akamuacha akaenda bila kusubiri shukurani kutoka kwa familia ya mtoto, na hapa kitendo chake hiki hakiwezi kuitwa kuwa alikuwa na shida au mchezo usio na faida, bali kitendo hiki ni ukarimu na ni roho nzuri, na tabia njema!
Hivyo, hakuna mafungamano kati ya kuhitaji na mchezo![14]
Na imekuja katika Sahihi Muslim, katika hadithil kudsi, kuwa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Enyi waja wangu laiti wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, binadamu wenu na majini wenu wakawa katika uchamungu wa moyo wa mtu mmoja miongoni mwenu, halitozidisha hilo chochote katika ufalme wangu, Enyi waja wangu, laiti wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu binadamu wenu na majini wenu wakawa katika uovu wa moyo wa mmoja wenu, halitopunguza hilo chochote katika ufalme wangu, Enyi waja wangu hakika haya (mnayoyafanya) ni matendo yenu, ninayakusanya kwa ajili yenu, kisha ninayalipa, hivyo, atakayepata kheri basi na amshukuru Mwenyezi Mungu na atakayepata kinyume na hivyo, basi asilaumu chochote ila nafsi yake"[15]
Mwenyezi Mungu hana haja na walimwengu.
Na harakati zetu na juhudi zetu na matendo yetu si ya mwingine bali ni kwa ajili ya nafsi zetu. "Na mwenye kupigana jihadi katika njia ya kuinua neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, na akapigana jihadi na nafsi yake kwa kuisukuma ifanye vitendo vya utiifu, basi anapigana jihadi kwa maslahi ya nafsi yake. Kwa kuwa yeye anafanya hilo kwa kutaka thawabu ya kupigana kwake jihadi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Hana haja ya matendo mema ya waja Wake" Suratul Ankabut: 61
Na sisi tunafahamu kuwa Mwenyezi Mungu ana hekima katika kila kuumba kwake, na mgonjwa kutojua hekima au maana ya daktari haimaanishi kuwa maamuzi ya daktari hayana maana.
Hivyo, kujua hekima za Mwenyezi Mungu hii haimaanishi ndio kuelewa hekima nzima kwa kiwango cha mwisho, bali inatosha kufahamu baadhi yake!.
Inatosha kujua kuwa sisi tumebebeshwa jukumu la sheria, na kujua uwepo wa hekima ya Mwenyezi Mungu, hii inatutosha kwa ujumla, vinginevyo tutakuwa sawa na anayepinga na kukufuru kila asichokielewa: "Bali wameyakanusha wasiyoyaelewa elimu yake kabla hayajawajia maelezo yake"
Hivyo Mwenyezi Mungu ni hakimu Mwenyezi hekima ya hali ya juu, na alituumba sisi kwa hekima yake Mtukufu.
Na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anayestahiki pekee kuabudiwa.

---

[12] Kitabu: Qisswatul Hadhwara, Will Durant, Juzuu ya 3 Uk. 209
[13] Chanzo kilichotangulia.
[14] Tazama kitabu: Dhwaahiratu naqdi ddini fil falsafatil hadiitha, cha Dr. Sultan Al Omairiy, ikiwa ni risala yake ya shahada ya Udaktari.
[15] Sahihi Muslim had. Na 2577

Hastahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, Yeye ndiye Muumba aliyetuleta sisi kutoka nakisichokuwepo, amesema Mtukufu: "Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale walio kabla yenu, ili mpate kuokoka". Suratul Baqara. Yeye ndiye aliyetuongoza na yeye ndiye aliweka sheria na akakadiria na akaamrisha na akakataza. "Alaah! Fahamuni! Kuumba na amri ni zake" [54] Suratul A'raf. Mwenyezi Mungu hamiliki kuumba pekee, bali amri zote ni zake pia na sisi tunaamrishwa kwa amri zake Mtukufu.

Ibada ndio haki ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake, kwa sababu yeye Mtukufu ndiye aliye tuumba, na akatuhuisha na akaturuzuku na akatuongoza na akatutumia Mitume wake, ili atutahini na atujaribu ni nani miongoni mwetu atakaye kuwa na matendo mema, hivyo, ibada ni haki ya Mwenyezi Mungu juu yetu. "Aliyeumba mauti na uhai ili awatahini nyinyi, enyi watu, ni yupi miongoni mwenu aliye mwema wa matendo na utakasaji wa nia? Na Yeye Ndiye Mshindi Ambaye hakuna chochote kinachomshinda, Ndiye Mwingi wa msamaha kwa anayetubia miongoni mwa waja Wake". Suratul Mulk. Na hayawezi kunyooka maisha yetu na akhera yetu isipokuwa kwa ibada, na haziwezi kutengemaa tabia zetu isipokuwa kwa ibada, ibada inakataza machafu na maovu na inatengemaa kwayo dunia ya watu, amesema Mola wetu Mtukufu: "Na usimamishe sala, hakika sala inakataza machafu na maovu". Suratul Ankabut: 45

Na wala hatuwezi kufuzu kuipata pepo ila kwa ibada, ndio muokozi katika akhera na ndio furaha ya dunia.

Ibada ni zetu sisi na ni kwa ajili ya mazuri yetu wenyewe, nayo ni wajibu upande wa Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na kutukuka, kwa sababu yeye ndiye aliyetuumba, na manufaa yake yanarudi kwetu sisi wenyewe, na uzembe ndani yake unarudi kwetu wenyewe.

Na pepo ni ghali (si rahisi) anayetaka pepo lazima afanye matendo kwa ajili ya kuipata, sisi ndio wahitaji kwake Yeye Mtukufu, tunaohitaji kumuabudu, naye ni mkwasi hana haja nasi na kila kiumbe chake.

## 21- Tutamjua vipi Mwenyezi Mungu?

Jawabu: Tunamjua Mwenyezi Mungu kwa njia nyingi sana, lakini tutataja hapa njia nne pekee:

Njia ya kwanza: Tunamjua Mwenyezi Mungu kwa njia ya maumbile salama (Moyo ambao haujaathiriwa na matamanio na akili ambayo haijaharibiwa na vikra potofu).

Mwanadamu kwa maumbile yake anajua kuwa anamuumbaji, wewe kwa maumbile yako mwenyewe unajua kuwa unamuumbaji aliyekuumba kwa umbo hili na kwa viungo hivi na umbile hili na ufundi huu na ufanisi wa kiwango cha juu.

Na pia mwanadamu kwa maumbile yake anajua kuwa yeye anatakiwa kurudi kwa muumba wake kwa kufanya ibada, na anajua pia kwa maumbile yake kuwa yeye ni muhitaji kwa muumba wake mtukufu na anamuhitajia kila wakati, na hisia hizi za uhitaji huongezeka wakati wa matatizo.

Hivyo, maumbile ya kumjua Mwenyezi Mungu ameumbiwa nayo kila mwanadamu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Basi simamisha uso wako, ewe Mtume, wewe na waliokufuata na uendelee kwenye msimamo wa dini ambayo Mwenyezi Mungu Amekuwekea, nayo ni Uislamu ambao Mwenyezi Mungu Ameufanya ulingane na maumbile ya watu. Basi kuendelea kwenu kubaki kwenye Uislamu, na kushikamana kwenu nao ni kushikamana na umbile la Mwenyezi Mungu la kumuamini Mwenyezi Mungu Peke Yake. Hapana ugeuzaji wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu na Dini Yake, kwani hiyo ndiyo njia iliyonyooka yenye kupelekea kwenye radhi za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe wote, na Pepo Yake. Lakini wengi wa watu hawajui kuwa yale niliyokuamrisha nayo, ewe Mtume, ndiyo Dini ya haki na si nyigine". Suratu Rum. Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na kumbuka, ewe Mtume, pindi Mola wako Alipowatoa wana wa Ādam kutoka kwenye migongo ya baba zao, Akawathibitishia upweke Wake kwa kuwatia tabia ya kimaumbile kwamba Yeye ni Mola wao, ni Muumba wao na ni Mmiliki wao; wakamkubalia hilo kwa kuchelea wasije kukanusha Siku ya Kiyama wasikubali chochote katika hilo na wasije wakadai kwamba hoja ya Mwenyezi Mungu haijasimama kwao na wala hawajui chochote juu yake, bali wao walikuwa wameghafilika na hilo". Suratul A'raf. Hivyo, kabla hatujaumbwa tulijengewa tabia ya kimaumbile ya kumtambua Mwenyezi Mungu, na tukaumbwa juu ya kumuabudu Yeye Mtukufu: "Na akawathibitishia upweke Wake kwa kuwatia tabia ya kimaumbile kwamba Yeye ni Mola wao, ni Muumba wao na ni Mmiliki wao; wakamkubalia hilo" Na amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- katika hadithi isiyo na shaka katika mapokezi yake: "Hakuna binadamu yeyote ila huzaliwa katika tabia ya maumbile"[16]

Sisi sote huzaliwa katika tabia hii ya maumbile, na maumbile haya yanamtosheleza kila mwanadamu mwenye kutaka haki kuyatumia kama ushahidi juu ya ukweli, na ajisalimishe kwa kuikubali haki hii wakati wowote itakapo mbainikia.

---

[16] Sahihi Muslim had. Na 2658

Na maumbile haya hawezi kuyapinga yeyote hata mpingaji mkubwa kuliko wote, hasa hasa katika nyakati ngumu za matatizo, watu wote hukimbilia kuomba msaada kwa Mwenyezi Mungu nyakati za matatizo, na husahau yale ambayo huyaabudu kama washirika wa Mwenyezi Mungu. "Na mkipatikana na shida baharini mkakaribia kuzama na kuangamia, wanapotea kwenye akili zenu wale waungu ambao mlikuwa mkiwaabudu, na mkamkumbuka Mwenyezi Mungu Muweza, Peke Yake, Awasaidie na Awaokoe, hapo mnamtakasia katika kutaka msaada na uokozi, na Yeye Anawasaidia na Anawaokoa. Anapowaokoa kwa kuwaegesha kwenye nchi kavu, mnageuka mkaacha Imani, kumtakasia Mwenyezi Mungu na matendo mema. Na huu ni katika ujinga wa binadamu na ukafiri wake, kwani binadamu ni mkanushaji sana neema za Mwenyezi Mungu, Aliyeshinda na kutukuka". Suratul Israa: 67.

Mwanadamu anapokuwa katika matatizo makubwa na akahisi kuangamia, basi kamwe hawezi kuomba mwingine zaidi ya Mwenyezi Mungu, na hapo atasahau washirika wake wote; Na huku kumtakasia Mwenyezi Mungu maombi wakati wa matatizo, msukumo wake mkubwa ni maumbile salama yanayopatikana ndani ya kila mwanadamu.

Anasema mmoja kati ya viongozi wa Amerika -Eisenhower- na alikuwa ni Jenerali wa Jeshi la Amerika katika vita vya pili vya dunia, anasema baada ya kushuhudia jinsi gani Jeshi linavyorejea katika maumbile ya asili wakati wa hatari kubwa: "Hawapatikani wapagani katika mahandaki"[17]

Ndani ya mahandaki wakati wa vita huwa hapatikani anayempinga Mwenyezi Mungu, watu wote hurudi kwa Mwenyezi Mungu, huu ndio uhalisia wa maumbile ambao watu wote wanaukubali wakati wa matatizo.

Njia ya pili ya kumfahamu Mwenyezi Mungu ni akili: Sisi tunamfahamu Mwenyezi Mungu kupitia akili. Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu "Je, wameumbwa bila kutokana na kitu chochote, au wao ndio waumbaji". Suratu Tur: 35.

Kwa akili ya kawaida, hapa inategemea mambo matatu na hakuna la nne yake:

La kwanza: Ima tuwe tuliumbwa bila muumbaji, kwa kauli yake " Je, waliumbwa bila kutokana na kitu chochote) na hili haliwezekani, yaani inawezekana vipi tuumbwe bila muumbaji?

La pili: Au tuwe tumejiumba wenyewe, kwa kauli yake "Au wao ndio wamejiumba" na hili haliwezekani pia, kwa sababu inawezekanaje nijiumbe mwenyewe kabla sijaumbwa?

Hivyo, kwa akili ya kawaida unabakia uwezekano wa tatu ambao aya imenyamaza haikuuzungumza, kwani unafahamika hata bila kwenda shule, nao ni kuwa tunaye muumbaji aliye tuumba.

Hivyo, sisi tunamjua Mwenyezi Mungu kupitia akili.

Njia ya tatu ya kumfahamu Mwenyezi Mungu ni kutazama katika viumbe vya Mwenyezi Mungu:

Hivyo, kutazama katika viumbe vya Mwenyezi Mungu kunatuweka sisi mbele ya utukufu wa Mwenyezi Mungu -Aliyetakasika na kutukuka- "Sema; Tazameni ni nini kilichoko mbinguni na ardhini" [101] Surat Yasin.

Kila tunapotazama katika ufanisi wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu na maajabu ya ufundi, tunazidisha maarifa ya kumjua Mwenyezi Mungu.

Na hili ndilo tulilolieleza awali katika ushahidi wa uumbaji na ushahidi wa kutilia manani na ufanisi.

Njia ya nne ya kumtambua Mwenyezi Mungu ni kupitia Mitume:

Na hii ndio njia kuu ya kumtambua Mwenyezi Mungu -Aliyetakasika na kutukuka-, Nayo ni sisi kumjua Mwenyezi Mungu kupitia Manabii na Mitume wake, Mitume walitoa habari za kumhusu Mwenyezi Mungu na za kuhusu sifa zake na wakaeleza kuhusu dhati yake Mtukufu, hivyo, kupitia Manabii tumemjua Mwenyezi Mungu kwa majina yake na sifa zake, na tumejua ni jinsi gani tutamuabudu Mwenyezi Mungu na tunajikurubisha kwake, na tumejua ni jinsi gani tutaokoka siku ya hesabu kutokana na adhabu ya Mwenyezi Mungu, hivyo, Mitume waliwaita watu kuja katika ibada ya Mwenyezi Mungu, au kwa maana nyingine: Waliwaita watu kurudi katika maumbile yao waliyoumbiwa nayo na wamuabudu Mwenyezi Mungu kama alivyoamrisha.

Hivyo, Mitume waliwaelekeza watu kuja katika njia ya haki na uokovu. "Nimewatuma wajumbe kwa viumbe wangu wakatoe habari njema ya malipo yangu mema na waonye juu ya adhabu yangu, ili wanadamu wasiwe na hoja watakayoifanya ni kisingizio cha udhuru baada ya kutumiliza Mitume. Na daima Mwenyezi Mungu ni Mshindi katika mamlaka Yake, ni Mwingi wa hekima katika uendeshaji mambo Wake". Suratun Nisaa [165]

Habari za Mitume na Manabii hawa kuhusu Mwenyezi Mungu na kupewa kwao msaada na Mwenyezi Mungu wa miujiza, ili asipate yeyote hoja juu ya Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama.

---

[17] https://en.wikipedia.org/wiki/There_are_no_atheists_in_foxholes

Mwenyezi Mungu Mtukufu amekupatia maumbile ambayo utaweza kumtambua muumba wako kupitia maumbile hayo, na akakupa akili na akakupa uwezo wa kutazama katika viumbe vyake na akakutumia Mitume, haijabakia hoja yoyote kwako kwa Mwenyezi Mungu.

## 22- Kuna dini nyingi sana, kwa nini iwe Uislamu pekee?

Jawabu: Uislamu si dini miongoni mwa dini nyingi.
Uislamu itikadi yake inakubaliana na itikadi ya Manabii wote wa agano la kale.
Hivyo, Uislamu ni masahihisho ya mapito ya dini zingine zilizopotoshwa, na ni kurudisha itikadi ya Manabii wa zama za kale ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada.
Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Amekupeni sheria ya Dini ile ile aliyomuusia Nuhu na tuliyo kufunulia wewe, na tuliyo wausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo. Ni magumu kwa washirikina hayo unayo waitia. Mwenyezi Mungu humteua kwake amtakaye, na humuongoa kwake aelekeaye". Suratu shuura: 11.
Hivyo, Uislamu si dini kama dini zingine bali ndio asili ya dini zote.

## 23- Uislamu ni nini?

Jawabu: Uislamu ni kujisalimisha na kunyenyekea na utiifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:
Amesema Mwenyezi Mungu -Aliyetukuka sifa zake-: "Hakuna yeyote aliye mwema wa dini kuliko yule aliyejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Peke Yake, kwa moyo wake na viungo vyake vyote, hali ya kuwa ni mwema wa maneno na vitendo, mwenye kufuata amri ya Mola wake, akawa amefuata mila ya Ibrāhīm na Sheria aliyoileta na amejiepusha na itikadi mbaya na sheria zilizo batili. Na Mwenyezi Mungu Alimteua Ibrāhīm, rehema na amani zimshukie, na akamfanya ni msafi Wake miongoni mwa viumbe Wake" Suratun Nisaa [125]
Na maana ya aliyejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu: Yaani: Akajisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na akatii kwake Aliyetakasika na kutukuka Mola wetu, na huyu ndiye mtu mwema zaidi wa dini.
Na alisema Allah Mtukufu: "Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimisheni kwake tu, na wape habari njema wanyenyekevu" Suratul Haji: 34.
Na maana ya jisalimisheni kwake tu: Yaaani; Jisalimisheni katika hukumu zake.
Aya hii inaonyesha kuwa maana ya Uislamu ni kujisalimisha moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kumtii Yeye Mtukufu na Aliyejuu, na kutekeleza sheria zake na njia yake kwa ridhaa na kukubali, na hiki ndicho kiini cha Uislamu.
Uislamu ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu katika maamuzi yake na sheria zake.
Na Uislamu ndio dini ya Mwenyezi Mungu kwa wanadamu wote, Amesema Mtukufu: "Hakika dini pekee mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu" [Surat Al Imrani: 85] Uislamu ndio dini pekee ambayo Mwenyezi Mungu hakubali dini nyingine isiyokuwa hiyo "Na Mwenye kutafuta dini isiyokuwa dini ya Kiislamu, basi hiyo haitakubaliwa kwake, na yeye Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye kupata hasara". [Surat Al Imrani: 85]
Na Uislamu ndio dini ambayo aliwatuma kwayo Mitume na Manabii wote, hivyo, dini ya Manabii ni moja nayo ni unyenyekevu (Uislamu), na Manabii wote walikuja na ujumbe wa kumpwekesha Mwenyezi Mungu, hata kama zitatofautiana sheria zao.
Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na hatukupata kutuma kabla yako, ewe Mtume, mjumbe yeyote isipokuwa tunampatia wahyi kwamba hapana mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu. Basi mtakasieni ibada Yeye Peke Yake". Suratul Anbiyaa: 25
Na haijabakia katika imani hii ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu peke yake isipokuwa dini ya Uislamu. Uislamu ndio dini ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu peke yake mpaka sasa juu ya mgongo wa ardhi. Kwani wote wenye kujinasibisha na sheria zingine, wamekuwa na ushirikina sawa sawa uwe kidogo au mwingi, baada ya kufa Manabii na baada yakuwa wamewaacha watu katika imani ya kumuabudu Mungu mmoja (Tauhidi) watu wakajifanyia ushirikina, na mpaka leo hii hakujabakia katika tauhidi safi waliyokuja nayo Manabii dini yoyote zaidi ya uislamu.

## 24- Je katika Uislamu kuna majibu ya maswali yaliyotatiza akili nyingi kuyajibu: Tulitoka wapi? Na kwanini sisi tuko hapa ulimwenguni? Na tunaelekea wapi?

Jawabu: Uislamu umeyajibu maswali yote haya katika aya moja tu katika Qur'ani Tukufu, amesema Mola wetu Mlezi Aliye takasika na kutukuka. «Na ni kitu gani kitakachonizuia mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu Aliyeniumba na Ambaye Kwake mtarejea nyote?" Suratu Yasin.
Ulitokea wapi? Mwenyezi Mungu ndiye aliye niumba.

Na ni wapi nitakwenda mimi? Nitakwenda kwa Mwenyezi Mungu ili nihesabiwe kwa matendo yangu, "Na kwake mtarejeshwa".
Kwa nini nilikuja katika dunia hii? Kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu na ili nipewe mitihani.
Kwa nini namuabudu Mwenyezi Mungu? Ni jambo la kawaida mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu aliye niumba, hii ni tabia ya mahusiano baina ya mja na Mola wake, kuwa mja amuabudu Mola wake na muumba wake. «Na ni kitu gani kitakachonizuia mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu Aliyeniumba?" Aya moja imekusanya majibu ya maswali matatu muhimu yanayo washinda binadamu kuyajibu. «Na ni kitu gani kitakachonizuia mimi kumuabudu Mwenyezi Mungu Aliyeniumba na Ambaye Kwake mtarejea nyote?" Suratu Yasin.

# 25- Nimejuaje kuwa Muhammadi -Rehema na amani ziwe juu yake- ni Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu?

Jawabu: Wingi wa ushahidi wa changamoto zilizotolewa na Qur'ani na zikawashinda watu wote, hii inamaanisha kuthibiti na ukweli wa taarifa usiokuwa na shaka.
Mwanafalsafa Arosto pamoja na kazi zake zote kwa ujumla alizozifanya lakini hakuna sentensi hata moja au ufumbuzi aliyowahi kuutoa wa kutatua maswali hayo.
Daktari Hippocrat pamoja na miradi yake yote ya udaktari lakini hakuna jeraha la maumivu ya maswali hayo aliwahi kulijibu.
Na vile vile kupatikana kwa dalili nyingi zilizotoa changamoto na zikanukuliwa kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kunaonyesha uhakika na yakini kamili ya habari zilizotufikia kuwa yeye ni Nabii.
Ukitazama katika historia yake -Rehema na amani ziwe juu yake- utakuta kuwa ni mkweli, na alijulikana kwa sifa ya ukweli kwa kukubalika na adui yake mkubwa, na hakuwahi kutuhumiwa kwa uongo wala uovu, kisha alikuwa akieleza mambo ya ghaibu kisha yanatokea kama alivyoeleza, na kabla ya hapo itikadi yake aliyoifundisha iliafikiana na itikadi ya Manabii wote, na yeye ndiye aliyetabiriwa na Manabii kuja kwake -Rehema na amani ziwe juu yake- kabla ya kuja kwake kwa mamia ya miaka, yote hii inamaanisha ukweli na uhakika wa taarifa juu ya ukweli wa utume wake.
Kisha tunaweza kusema nini kuhusu muujiza mkubwa zaidi aliokuja nayo ambao ni Qur'ani?
Qur'ani ambayo alitoa changamoto Mwenyezi Mungu kwa watu mafasaha, kuwa walete mfano wake au sura moja miongoni mwake, lakini hawakuweza.
Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hamkuweza na kamwe hamtoweza" [24] Suratul Baqara.
Hawakufanya na wala hawakuweza.
Na bado Qur'ani tukufu inaendelea kuwapa changamoto wasomi wakubwa wakishirikina na mafasaha wakubwa, nao pamoja na yote waliyonayo wameshindwa kuleta upinzani, hawawezi kuleta mfano wake.
Anasema Dr. Abdallah Draz -Mwenyezi Mungu amrehemu: "Hivi hakuhofia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu changamoto hii kuamsha hisia zao za kisomi?
Wakamiminika na kuungana kushindana naye, hivi unadhani ni nini angeweza kufanya laiti kundi la wasomi wakubwa wangekubaliana kutoa maneno yenye kufanana hayo hata katika baadhi ya sehemu zake!
Kisha laiti nafsi yake ingemtuma kutoa hukumu hii kwa watu wa zama zake angewezaje kuitoa katika vizazi vijavyo?
Hakika balaa hili hawezi kulivaa isipokuwa mtu anayejua nafasi ya nafsi yake, na amejawa na ujuzi wa mabadiliko ya kuhukumu, na habari zitokazo mbinguni, na hivi ndivyo alivyoiweka juu ya mgongo wa Ardhi, ikawa ndio hukumu iliyopangiliwa, kila aliyepingana naye alikumbana na kushindwa wazi wazi, na fedheha ya kufeli, kwa zama zote milele[18]
Washirikina hawa waliona kuwa kukusanya majeshi na kuandaa makundi kwa ajili ya kumpinga vita Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ndilo jambo rahisi na jepesi kuliko kupingana na Qur'ani na kukubali changamoto, na hapa ndipo zilipoishia juhudi zao. "Na waliokufuru walisema: Msiisikilize hii Qur’an, na timueni zogo huenda mkashinda". [Fuswilat: 26].
Waarabu wote, bali hata umma mmoja ulioletewa changamoto hii haukuweza kuleta kitu chochote ambacho watakikubali wapagani na watawaridhisha watu wengine.
Anasema Al-Alusi -Mwenyezi Mungu amrehemu-: "Hakuwahi kuzungumza yeyote miongoni mwao mpaka leo hii kwa kinywa chake wala kutengeneza sentensi yenye mfumo au sifa kama ya Qur'ani".
Amesema Jubairi bin Mutwi'm na alikuwa bado hajasilimu: "Nilimsikia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akisoma katika swala ya Magharibi suratu ttur, alipofikia aya hii: "Je, wameumbwa bila kutokana na

[18] Kitabu: Annabaul Adhwiim. Dr. Abdallah Draz -Mwenyezi Mungu amrehemu, uk 44-45.

kitu chochote, au wao ndio waumbaji". "Au wao wameumba mbingu na ardhi kwa utengenezaji huu wa kipekee? Bali wao hawaamini adhabu ya Mwenyezi Mungu, kwa kuwa wao ni washirikina". "Au wanazo wao hazina za Mola wako wanazitumia? Au wao ni majabari wanaowagandamiza viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa kuwatenza nguvu na kuwanyanyasa? Mambo si hivyo, bali wao ndio waelemevu walio madhaifu". Suratu Tur: 35.
Anasema: "Moyo wangu ulikaribia kuruka"[19]
Qur'ani ndani yake kuna siri za ajabu, zinazoweza kupenya ndani ya nafsi ya mtu.
Tafakari jinsi gani wanawake wa kishirikina walivyokuwa wakija kwa wingi katika nyumba ya Abubakari alipokuwa akisoma Qur'ani, ni jinsi gani walivyokuwa wakivutika na wakiathirika nayo, mpaka likawashangaza mno swala hilo wanaume wa kikureishi[20]
Na kwa ajili hii ulikubaliana umoja wa warabu kuwa wasiisikilize Qur'ani wala wasiwasikilizishe familia zao, hii ndio njia pekee ya kubakia katika ukafiri.
Na miongoni mwa maajabu makubwa ya Qur'ani tukufu na miujiza yake isiyomalizika ni yale aliyoyaeleza Dr. Abdallah Draz -Mwenyezi Mungu amrehemu- katika swala la kuteremka kwa aya za Qur'ani kwa nyakati tofauti tofauti, kisha anaelekeza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake kuziweka baadhi ya aya katika maeneo maalum baina ya sura na aya zingine, kisha mwisho kila sura inaonekana ikiwa imekamilika mithili ya jengo lenye kujitegemea, anasema Mwenyezi Mungu amrehemu: "Na wakati wa kuteremka Qur'ani baadhi ya sehemu za Qur'ani zilikuwa zikiongezeka kivyake nje na sehemu zingine, na zikitengeneza kidogo kidogo vifungu vya kujitegemea baada ya kuungana na aya zingine zilizoteremka baada yake, kulingana na amri ya Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- aliyokuwa akiipokea kwa nafasi yake kutoka kwa Roho Mtakatifu (Jibrili).
Kwa mfano tukichukua historia isiyo na kikomo -historia ya kuteremka Qur'ani Tukufu, na tukagundua kuwa Ufunuo (Wahyi) huu kwa ujumla ulikuwa umefungamana na hali na matukio maalum, basi hilo linatulazimu kujiuliza kuhusu wakati ambao ilikamilika kazi hii ya kupangilia kila sura kwa namna ya kipekee na ya kujitegemea.
Hii ni kana kwamba Qur'ani hakika haikuwa mahala pamoja na haikuwa imeandikwa kwa mpangilio tangu zamani, ni kama ilikuwa inarudiwa kuundwa kwake katika mahala pengine kwa mfumo huo huo uliotangulia, nje na hapo, tunawezaje kuufasiri utaratibu huu wa haraka na wa kitaaluma kwa wakati mmoja, kwa yanayohusiana zaidi na sura hizi nyingi?
Lakini ni dhamana ipi ya kihistoria anayoweza kuipata mwanadamu wakati uwekaji wa mpango huu, ukilinganisha na kila tukio kufanyika kwa wakati wake, na mahitaji yake ya kisheria, na suluhisho sahihi kwake, ukiachilia mbali muundo wa lugha unaotakiwa kutoa suluhisho la hili, na uendane na utaratibu kama huu, ili uwe badala ya huu wa Qur'ani?
Hivi, hatutaki kupata matokeo yakuwa kukamilika kwa mpangilio huu na kutimia kwake kwa namna inayotarajiwa, kuwa swala hili linalazimu kuwa na mchango wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani yake, ambaye uko kwake uwezo huu wa kuweka huu mpangilio uliokusudiwa?"[21]
Qur'ani ni muujiza wa kipekee wa juu ya ukweli wa utume wake -Rehema na amani ziwe juu yake-.
Na miujiza yake -Rehema na amani ziwe juu yake- iliyotokea mbele yake ni mingi mno, ni zaidi ya elfu moja, na zama hazikupita wakawa wameinukuu watu ambao ndio viumbe wakweli zaidi na wema zaidi.
Na hawa wapokezi walioripoti kwetu miujiza hii, walikuwa hawakubaliani na uongo hata katika mambo madogo zaidi, je, watawezaje kumuongopea, hali yakuwa wanajua kuwa yeyote mwenye kumsemea uongo basi ajiandalie makazi yake motoni!, kama alivyotahadharisha yeye mwenyewe -Rehema na amani ziwe juu yake-.
Na baadhi ya miujiza yake -Rehema na amani ziwe juu yake- waliishuhudia maelfu ya wanafunzi wake, na baadhi yake waliipokea makumi miongoni mwao, inawezekanaje wote wakubaliane kusema uongo katika haya yote?!
Na mfano katika miujiza yake ambayo waliishuhudia kundi kubwa la watu: Tukio la mnung'uniko wa gogo la mti, ambayo ni historia mashuhuri iliyopokelewa bila ya shaka, wakati ambao alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akihutubu akiwa juu ya gogo la mti, alipotengenezewa mimbari gogo lilimlilia, na likalia mithili ya kilio cha mtoto mdogo, likaendelea kulia mpaka akalikumbatia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, hapo likanyamaza.

---

[19] Sahihi Bukhari, Hadithi na: 4854.
[20] Sahihi Bukhari, Hadithi na: 3905.
[21] Kitabu: Mad-khal Ilal Qur'anil Kariim, cha Dr. Abdallah Draz.

Na tukio hili (hadithi) hii walioipokea miongoni mwa masahaba ni: Anasi bin Maliki, Jabiri bin Abdillah, na Abdallah bin Abbasi, na Abdallah bin Omari, na Ubaiya bin Ka'bu, Abii Saidi, na Sahli bin Saidi, na Aisha binti Abubakari, na Ummu Salama.
Je, mfano wa idadi kama hii ya masahaba wanaweza kukubaliana uongo katika kupokea habari kama hii?.
Bali baadhi ya miujiza yake waliishuhudia maelfu ya masahaba mfano: Chemchem ya maji katika vidole vyake vitukufu, iliyobugujika mpaka wakatawadha kutoka katika maji hayo na wakanywa masahaba elfu moja na mia tano, na hadithi inamapokezi yasiyo na shaka, kaipokea Bukhari na Muslim.
Na kukifanya chakula kidogo kuwa kingi, wakala jeshi kubwa, na muujiza huu taarifa yake imepokelewa na watu wengi na haina shaka kutoka kwa masahaba, na ameeleza Bukhari peke yake miujiza ya kukifanya chakula kuwa kingi kupitia mkono wa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- katika maeneo matano katika Sahihi yake[22].
Ikiwa ushahidi wa ukweli umethibiti na miujiza mingi ya kutosha kuhusu utume wake -Rehema na amani ziwe juu yake-, inawezekana vipi mtu mwenye akili kukanusha yote hii?
Hii hapa mifano mingine ya miujiza yake -Rehema na amani ziwe juu yake-:
Alieleza -Rehema na amani ziwe juu yake- usiku miongoni mwa siku kuwa upepo mkali utavuma usiku, na akawakataza watu kuamka, mtu mmoja akaamka na akatoka nje upepo ukambeba na kumtupa sehemu ya mbali kutoka nyumbani kwake.[23]
Na alieleza -Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu kifo cha Mfalme Najashi katika siku aliyokufa, na akatoa takbira nne (Akasema Allahu Akbar mara nne)[24]
Na alieleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuhusu vifo vya kufa mashahidi, Masahaba kama, Omari Othman, na Ally na Twalha na Zubairi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote, nakuwa hawatofia katika vitanda vyao kama wanavyokufa watu wengine.
Alipanda mlima Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- siku moja akiwa yeye na Abubakari na Omari na Othman na Ally na Twalha na Zubairi, Mwamba ukatikisika, akasema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuliambia Jabali: "Tulia, hapa uko na ima Nabii au sidiki (waliomkubali Mtume) au shahidi"[25]
Akatoa hukumu juu ya nafsi yake kuwa ni Mtume na kwa Abubakari kuwa ni sidiki (Aliyemsadikisha Mtume) na kwa waliobakia kuwa watakufa mashahidi, na yakatokea aliyoyaeleza -Rehema na amani ziwe juu yake-.
Na kuna hadithi takribani mia moja na hamsini (150) aliwaombea Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kwa Mola wake na zikajibiwa papo hapo na watu wakishuhudia!.[26]
Na pindi walipomtaka Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-wakazi wa Makka awaonyeshe muujiza, basi akaupasua mwezi vipande viwili, mpaka wakaona uwazi kati yake, na hadithi hii imepokelewa kwa mapokezi yasiyo na shaka, yaani iko katika daraja ya juu zaidi ya usahihi.
Na alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akisoma suratul Qamari ambayo ndani yake kuna muujiza wa kupasuka mwezi katika makongamano makubwa kama sala za ijumaa na sikukuu za Idd, ili awasikilizishe watu yale yaliyomo miongoni mwa miujiza yake -Rehema na amani ziwe juu yake- na alikuwa akiitumia kama ushahidi wa kuthibitisha ukweli wa unabii wake.
Kisha kueleza kwake Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa Adamu ndiye kiumbe wa mwisho kuumbwa katika viumbe hai:"Na Mwenyezi Mungu alimuumba Adamu baada ya Alaasiri katika siku ya Ijumaa: naye ni kiumbe wa mwisho".[27]
Na uhalisia huu wa kisomi leo umethibiti, alijuaje -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa Adamu -Amani iwe juu yake- ndiye kiumbe wa mwisho kuumbwa juu ya mgongo wa Ardhi baada ya kudhihiri kwa mimea na wanyama?.
Hebu tazama na utafakari kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. "Na tumeufanya usiku na mchana kuwa ni alama mbili, tukaifuta alama ya usiku na tukaweka alama ya mchana ili iwe ni mwangaza" Suratul Israa: 12.

---

[22] Bukhari (1217) Bukhari (2618) Bukhari (3578), Bukhari (4101), Bukhari (6452). Na yote ni matukio na visa tofauti tofauti, na hii ni katika Sahihi Bukhari pekee!.
[23] Sahihi Muslim: Hadithi na: 3319.
[24] Sahihi Bukhari, Hadithi na: 1333.
[25] Sahihi Muslim had. Na 2417
[26] Amezikusanya hadithi hizi zote Saidi bin Abdil Qadiri Bashfar, katika kitabu chake Dalaailun nubuwwa, na kitabu kimechapishwa na Daru bin Hazmi.
[27] Sahihul Jaami, 8188.

Tukaifuta alama ya usiku: Yaani Mwezi ambao ndio alama ya usiku ulikuwa ukiangaza kisha ukafutwa mwangaza wake.
Na hivi, hakika ndivyo walivyofasiri masahaba aya tukufu, amepokea imamu bin Kathiri katika tafsiri yake yakuwa Abdallah bin Abbasi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: "Mwezi ulikuwa ukiangaza kama linavyoangaza Jua, ambao ndio alama ya usiku, ukafutwa".
Na cha ajabu zaidi nikuwa hapo ndipo walipofikia wanasayansi wa zama hizi, walichapisha baadhi ya watu katika tovuti zao na chaneli zao za televisheni: Kuwa kipindi cha mwanzo mwezi ulikuwa na mwangaza mkali zaidi ya hivi sasa.[28]
Na imethibiti kwa habari za uhakika kutokea kwa miujiza na taarifa za mambo ya ghaibu, na habari za ndani zaidi za siri za Ardhi na Mbingu zisizokuwa na idadi, yote haya yakitoka kwa mtu mmoja -Rehema na amani ziwe juu yake-, na kuteremka kwa Qur'ani juu yake, na akaja na habari zile walizokuwa nazo Manabii kabla yake, na alikuwa na uungwaji mkono kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na hakufa mpaka ilipotimia sheria na ikakamilika.
Kukubali bila utata kuwa yeye ni Nabii ndio usawa unaokubaliana na akili!.
Miujiza yake -Rehema na amani ziwe juu yake- ya ghaibu iko zaidi ya elfu moja.
Na walioripoti miujiza yake ni wanafunzi wake ambao ni viumbe wakweli na wema zaidi baada yake.
Na cha ajabu nikuwa masahaba wakubwa waliukubali Uislamu kabla hata ya kuona miujiza, walisilimu kwa sababu walijua kuwa Nabii Muhammadi -Rehema na amani ziwe juu yake- ni mkweli, na kwamba hakuwahi kusema uongo kamwe kabla ya hapo.
Na msimamo huu waliouchukua masahaba wakubwa ndio msimamo wa akili na busara, ukweli wa Nabii -Rehema na amani ziwe juu yake- ni dalili tosha ya kuthibitisha unabii. Na hii ni kwa sababu: Mtu anayedai unabii ni mmoja: Ima awe mtu mkweli kuliko wote, kwa sababu yeye ni Nabii. Na Nabii yeye ndiye mtu mkweli kuliko watu wote.
Na ima awe: Muongo kuliko wote, kwa sababu anazua uongo katika jambo zito na kubwa kuliko yote.
Na hawezi kuwatatiza watu mtu muongo na mkweli wakashindwa kuwatofautisha ila kwa mjinga kuliko watu wote.[29]
Ni rahisi sana mwenye akili kutofautisha kati ya mtu mkweli zaidi na muongo zaidi.
Na walikubali washirikina tangu mwanzo tu wa utume wake -Rehema na amani ziwe juu yake- yakuwa hakuwahi kusema uongo kamwe, wakasema: "Hatujawahi kupata uongo kutoka kwako"[30].
Na pindi alipomuuliza Hirakli Abuu Sufiani kabla hajasilimu: "Je, hivi mlishawahi kumtuhumu kwa uongo kabla hajasema hayo aliyoyasema?".
Abuu Sufiyan akasema: "Hapana".
Hirakli akasema: "Asingeweza kuacha kuwadanganya watu halafu aweze kumsemea uongo Mwenyezi Mungu".
Kisha akamaliza mazungumzo Hirakli akasema kauli yake maarufu: "Laiti ningekuwa naishi pamoja naye basi ningeosha miguu yake" (Ningemtii kwa lolote, hata ikiwezekana kuosha miguu yake)[31]
Makafiri walishindwa kuonyesha uongo hata mmoja katika maisha yake yote -Rehema na amani ziwe juu yake-, na ndio maana Qur'ani ilikemea kupinga kwao huku pamoja nakuwa wanajua hali yake kabla ya kuwa Mtume, akasema Mola wetu Mtukufu: "Au limewazuia wao kuifuata haki kwa kuwa Mtume wao, Muhammadi, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie, hajulikani kwao na kwa hivyo wanamkataa?" Suratul Muuminuun: 69
Hali ya Mtume na historia yake ndio dalili ya mustakabali kuwa yeye ni Nabii.
Rehma na amani za Allah ziwe juu yake
Ikiwa vigezo vya ukweli kwa ujumla vyote vinaungana juu ya utume wake -Rehema na amani ziwe juu yake-, inawezekana vipi mtu mwenye akili kukanusha yote hii?

# 26- Ninawezaje kujua kuwa mimi ninatakiwa kumuamini Mwenyezi Mungu?

Jawabu: Jichunguze mwenyewe utabaini kuwa wewe umepewa mtihani, kwani ndani ya mwili wako hakuna hisia zinazokutuma kuwa; Fanya jema, na usifanye kosa?

---

[28] http://www.nasa.gov/mission_pages/LRO/news/vid-tour.html
https://www.youtube.com/watch?v=UIKmSQqp8w
[29] Tazama kitabu: Thubutun nubuwwa Aqlan wanaqlan, cha bin Taimia, chapa ya Daru binil Jauzi, uk 573, na maana yake pia iko katika kitabu hicho hicho uk 318.
[30] Sahihi Bukhari, Hadithi na: 4971.
[31] Sahihi Bukhari, Hadithi na: 7.

Mfano: Mbele yako kukiwa na mali na mwenye nazo hana habari nazo, kimaumbile zitakuijia hisia kuwa chukua mali hizo na ufaidike nazo, lakini hisia zingine zinakutuma: Hapana, usifanye hivyo, hili ni marufuku na ni kosa.
Hivyo, wewe ni mtahiniwa katika kila mahali maishani mwako.
Hisia hizi za -Fanya na usifanye- zinapatikana ndani ya mwili wako kwa sababu wewe ni mtahiniwa na wala hujaachwa bura, wewe si kitu kilichotelekezwa hovyo bila ya thamani.
Amesema Mtukufu: "Sisi tumembainishia na kumfahamisha njia ya uongofu na upotevu na wema na ubaya ili awe ima ni mwenye kuamini na kushukuru. Au awe ni mwenye kukanusha na kukataa". Suratul Insan: 3
Mwanadamu ndani ya mwili wake kuna "Fanya na usifanye": Hivyo huwa katika moja kati ya hali mbili katika maisha yake, ima ashukuru au akufuru.
Bali katika kila hatua miongoni mwa hatua za maisha ya mwanadamu inawezekana mwanadamu kufanya kheri au kufanya shari, je, aende msikitini au aende katika upuuzi.
Na kwa sababu hiyo amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Sikuumba majini wala watu ila ni kwa lengo la kuniabudu" Suratudh-dhariyat: 56.
Katika kila hatua utapata aina miongoni mwa aina za kumuabudu Mwenyezi Mungu au kumuasi Yeye Mtukufu.
Yeyote atakayepewa taufiki katika jambo fulani aliloliamrisha Mwenyezi Mungu basi atakuwa kaokoka, na atakayeasi aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu basi atakuwa katenda kosa.
Na uhuru huu wa maamuzi unaambatana na hesabu juu ya mwanadamu kwa kila alilolifanya.
Hivyo, lengo la kuumbwa kwetu ni kupewa mtihani na majaribu, na hili ndilo lengo ambalo Mwenyezi Mungu aliwatuma Mitume kwa ajili yake na akateremsha vitabu "Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani". [An nahli: 36]
Na baada ya kumalizika mitihani kwa kifo tunarudi kwa Mwenyezi Mungu "Na kwake mtarejeshwa" [Suratu Yassin: 22]
"Na kwamba mwisho (wa kila jambo) unarejea kwa Mola wako" Suratun Najmi: 42 "Hakika kwa Mola wako Mlezi ndio marejeo" Suratul Alaq: 8 Hivyo, sisi tutarudi kwa Mwenyezi Mungu ili tuhesabiwe kwa yale tuliyoyatanguliza "Na kwamba amali yake itaonekana" "Kisha atalipwa malipo yaliyo kamili" Suratun Najmi: 40-41 Yataonekana yote uliyoyatanguliza katika matendo na utahesabiwa kwa hayo. "Yeyote mwenye kufanya jema uzito wa mdudu chungu mdogo atayaona malipo yake Akhera" (7) Na yeyote mwenye kufanya baya uzito wa punje ndogo atayaona malipo yake Akhera (8) Suratulz zilzala 7-8.

# 27- Je, inatosha kumwamini Mwenyezi Mungu na kuwapinga Manabii?

Jibu: Hapana!
Kuamini uwepo wa Mwenyezi Mungu pamoja na kutowaamini Manabii, hii haitoshi mpaka mwanadamu ajisalimishe kwa Mwenyezi Mungu, inamaana gani kumuamini Mwenyezi Mungu kuwa Yeye ndiye Muumbaji na Mpangiliaji, kisha unapinga ufunuo wake na unawapinga Mitume wake?
Huu ni ukafiri mkubwa.
Bali hakuna uhalifu mkubwa kuliko huyu anaye ukataa ufunuo wa Mwenyezi Mungu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hakika wanaomkanusha Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, kati ya Mayahudi na Wanaswara, na kutaka kutenganisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, kwa kumuamini kwao Mwenyezi Mungu na kuwakanusha Mitume Wake Aliowatuma kwa viumbe Wake, au wautambue ukweli wa baadhi ya Mitume na kuacha kuwatambua wengine na wadai kwamba baadhi yao wamemzulia Mola wao urongo na wanataka kujifanyia njia ya kuelekea kwenye upotofu waliouanzisha na uzushi waliouzua. Hao ndio wenye ukafiri wa hakika usiokuwa na shaka. Na tumewaandalia makafiri adhabu itakayowadhalilisha na kuwatweza". Suratun Nisaa [165]
Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na akawakanusha Manabii basi huyo ni kafiri wa kweli.
Yeyote mwenye kumkanusha Nabii miongoni mwa Manabii huyu kamkanusha Mwenyezi Mungu, kwa sababu yeye kakanusha ufunuo wa Mwenyezi Mungu, ndio maana Wakristo na Mayahudi walikufuru kwa sababu ya kukanusha kwao utume wa Muhammadi bin Abdillah -Rehema na amani ziwe juu yake- "Hakika wale waliokufuru miongoni mwa Mayahudi na Wanaswara na Washirikina, mateso yao ni Moto wa Jahanamu. Watakuwa ni wenye kukaa milele humo. Wao ndio viumbe waovu kabisa". Suratul Bayyina: 6.
Na ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuingia kwao motoni ni ya kweli "Hiyo, ni ahadi ya kweli" Suratu Qaf: 14.

Hivyo, Uislamu na kuokoka hakuwi kwa mtu kukiri kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Muumbaji Mtoa riziki Mwenye kuhuisha na kufisha pekee, bali ni lazima kuwamini Mitume wake.
Hivyo, kuamini uwepo wa Mwenyezi Mungu na kuwakanusha Manabii hakutoshi wala hakumnufaishi mja mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama, kwani ni lazima aabudiwe Mwenyezi Mungu na imani itimie kupitia Mitume wake wote.
Na lau kama kumuamini Mwenyezi Mungu pekee kungekuwa kunatosha, basi Mwenyezi Mungu asingelituma Mitume wake na wala asingeliteremsha vitabu vyake, kwa sababu watu wote wanamfahamu Mwenyezi Mungu kupitia maumbile yao ya asili.
Mwenyezi Mungu aliyekuumba wewe na akakuongoza na akakuruzuku Yeye pekee ndiye anayestahiki wewe umuabudu kama alivyoelekeza kupitia Mitume wake na Manabii wake.

# 28- Je kafiri anapata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya matendo yake mema?

Jawabu: Matendo mema ni maumbile aliyowaumba nayo Mwenyezi Mungu watu wote, ndio maana unaona kila mwanadamu anauwezekano wa kutenda mema hata kama ni kafiri au mshirikina, watu wote hufanya matendo mema kulingana na maumbile waliyoumbwa nayo.
Lakini sharti la kukubalika kwa matendo mema ni: Lengo liwe kupata radhi za Mwenyezi Mungu, yaani: lengo liwe kupata thawabu zake kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
Hivyo basi, mtu mwenye kumkufuru Mwenyezi Mungu mwenye kuabudu pamoja na Mwenyezi Mungu miungu mingine huyu tunamwambia: Nenda kwa wale uliowafanya kuwa washirika wa Mwenyezi Mungu katika matendo yako mema na kachukue malipo yako toka kwao, wewe hukutaraji kwa matendo yako haya mema kupata radhi za Mwenyezi Mungu pekee.
Vuta picha! Mtu kalelewa na familia yake vizuri na wakamhudumia kila kitu mpaka akawa kijana mwenye nguvu, kisha anakwenda kuwahudumia watu wa familia nyingine, hivi inaingia akilini kurudi nyumbani kwa familia yake na kuwambia: Nipeni malipo ya utumishi wangu niliowatumikia watu wengine!?.
Aende kwa wale aliokuwa akiwatumikia akachukue malipo yake kutoka kwao.
Na Mwenyezi Mungu anamfano wa juu zaidi kuliko huu.
Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuumba na akakupa riziki na akakuneemesha kwa kila aina ya neema, kisha unaacha kumuabudu na unataka uchukue malipo ya kazi yako kwake? Linawezekana vipi hili?
Na kwa sababu hiyo amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hapo tutayaleta yale waliyoyafanya yanayoonekana kuwa ni mazuri na ya kidini, tuyafanye ni yenye kubatilika na kupotea. Hayatawanufaisha na yatakuwa ni kama vumbi linalorushwa, nalo ni lile vumbi lembamba linaloonekana kwenye mwangaza wa jua. Hivyo ni kwamba matendo mema hayawi na manufaa yoyote huko Akhera isipokuwa mwenye kuyafanya awe na imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu na kumtakasia na kumfuata Mtume Wake Muhammadi, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie. Suratul Furqan: 23. Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na walio kufuru vitendo vyao ni kama sarabi (Mazigazi au Mangate) uwandani. Mwenye kiu huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote." Suratun Nur: 39.
Waliokufuru hawastahiki thawabu juu ya matendo hata kama yatakuwa mema, kwa sababu wao ni makafiri hawakukusudia kupitia matendo yao mema wapate thawabu za Mola wao Mlezi, wala hawakutaka radhi za Muumba wao kupitia matendo yao.
Swala la msingi si kufanya tu matendo mema, sisi sote tumeumbwa kuyaelekea matendo mengi mema, bali swala la msingi ni kwa nini unafanya jambo hili jema, na unalifanya kwa ajili ya nani? Je, unalifanya kwa ajili ya masilahi yako binafsi au unalifanya kutaka kuonekana au unalifanya kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu?
Yote haya hayako katika njia ya Mwenyezi Mungu na wala hayatarajiwi kuyapatia malipo ya matendo mema yanayotarajiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

# 29- Ikiwa Uislamu ni dini ya haki kweli, kwa nini kunapatikana utata ndani yake?

Jawabu: Utata unakuja katika baadhi ya mambo asiyoyaelewa muislamu katika dini yake, na yanaweza kumtatiza mpaka atakapoyapatia majibu.
Na Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka kuwe na mambo yenye kutatiza katika mambo ya sheria ya dini, ili ajiweke mbali nayo mwenye lengo baya la kutanguliza batili kuliko utiifu wa Mola wake Mlezi.
Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Yeye Peke Yake Ndiye Ambaye Aliyekuteremshia Qur’ani ambayo katika hiyo kuna aya zenye maana iliyo wazi; hizo ndizo msingi wa Kitabu ambao unategemewa ikitokea tashwishi, na ambao chochote kinachohalifiana nao kinarudishwa na kuoanishwa nao. Na katika hiyo kuna aya zingine mutashabihat: zinazoleta tashwishi kwa kuwa zinabeba zaidi ya maana moja, kwa

namna ambayo haiwezekani kujua maana iliyokusudiwa isipokuwa kwa kuziambatanisha na muhkam: aya zenye maana iliyo wazi. Basi wenye nyoyo zenye ugonjwa zilizopotoka, kwa ubaya wa nia zao, huzifuata hizi aya zenye tashwishi peke yake, ili kutia tashwishi kwa watu kwa lengo la kuwapoteza kwa kuzifasiri kuambatana na madhehebu yao yaliyo batili. Ilihali hakuna ajuwaye uhakika wa maana ya aya hizi isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na wale waliozama kwenye elimu wanasema, «Tumeiamini hii Qur'ani, kwani yote imetujia kutoka kwa Mola wetu kwa ulimi wa Mtume Wake Muhammad , Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie,.» na wanairudisha yenye tashwishi katika Qur'ani na kuioanisha na iliyo wazi yake. Hakika ni kwamba wanaoyafahamu na kuzingatia maana kama ilivyo sahihi ipasavyo ni wale wenye akili timamu". [Surat Al Imrani: 85]

Ama wale ambayo kwenye mioyo yao kuna maradhi hufuata yale ambayo yanatashwishi ndani yake: Yaani: Mwenye maradhi moyoni atafuata tashwishi hizi kwa lengo la kutafuta fitina na kutafuta kujiweka mbali na Mwenyezi Mungu.

Alitaka Mwenyezi Mungu kwa hekima zake kuwe na imani na ukafiri. "Wako miongoni mwenu ni makafiri na wako miongoni mwenu ni waumini" Suratut Taghabun: 2.

Hushikamana na tashwishi hizi mwenye kutaka ukafiri na kushughulika nazo kuliko hata dini yake na swala yake na imani yake.

Ama muumini hufuata dalili za wazi zilizothibiti na ambazo ndio (Mama wa kitabu) katika usahihi wa dini na utume, hata akipata jambo asilolifahamu basi huuliza, lakini hajishughulishi na yale asiyoyafahamu kuhusu dini yake au swala yake.

Hajishughulishi na asiyoyafahamu akaacha dini yake isipokuwa mtu mwenye maradhi moyoni mwake.

"Na wapate kusema wenye maradhi katika nyoyo zao na makafiri: Mwenyezi Mungu amekusudia nini kwa mfano huu? Ndiyo kama hivyo Mwenyezi Mungu humuacha apotee amtakaye, na humuongoza amtakaye" Suratu Mudathiri: 31.

Na katika hekima za kuwepo kwa utata pia nikuwa tashwisihi hizi hutofautisha wasomi wenye elimu katika dini ya Mwenyezi Mungu, utakuta msomi anajua jawabu la mambo yanayotatiza, na kati ya mtu asiye na elimu ambaye hajazama zaidi katika dini na wala hajaisoma, hapo Mwenyezi Mungu huwapandisha wasomi daraja ya juu zaidi.

Haki iko wazi lakini ni lazima kupatikane yenye kutatiza kwa sababu ndio huleta upembuzi kati ya watu na watu.

Utaratibu wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake ni kuwapa majukumu, na utaratibu wake katika majukumu ni kuwaficha baadhi ya hekima, na mshindi ni yule atakayetumia anayoyafahamu kama ushahidi wa yale asiyoyafahamu ya ndani zaidi, na aliyepata hasara ni yule aliyefanya asiyoyafahamu kuwa ni hoja ya kumzuia kuyatumia anayoyafahamu kama ushahidi.

# 30- Kwa nini Mwenyezi Mungu aliumba shari? Au kwa maana nyingine: "Anajibu vipi muislamu kuhusu shari yenye kutaabisha"?

Jawabu: Shari ndio sababu kubwa takriban ya upagani katika historia yote.

"Miongoni mwa watu kuna anayeingia kwenye Uislamu kwa udhaifu na shaka, akawa anamuabudu Mwenyezi Mungu juu ya shaka na ukosefu wa uamuzi, ni kama yule anayesimama kwenye ukingo wa jabali au ukuta, hawi thabiti katika kusimama kwake, huifungamanisha Imani yake na ulimwengu wake: akiishi katika hali ya afya na ukunjufu huendelea kwenye ibada yake, na akipatikana na mitihani ya tabu na shida huyanasibisha hayo na Dini yake, na kwa hivyo huiacha. Ni kama yule anayegeuka kwa uso wake baada ya kulingana sawa, hivyo basi akapata hasara ya ulimwengu, kwani kukufuru kwake hakugeuzi chochote alichokadiriwa katika ulimwengu wake, na akapata hasara ya Akhera kwa kuingia Motoni, na hiyo ni hasara inayoonekana waziwazi". Suratul Haji: 34.

Kuna mwenye kumkufuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ya mitihani au balaa au msiba uliompata.

Na hapo anaweza kuuliza mpingaji (Mpagani) na kusema: Kimsingi kwa nini kuwe na shari?

Na jibu ni jepesi: Kwa sababu sisi tumepewa majukumu.

Kwa sababu sisi tuko katika ulimwengu wa mitihani.

Amesema Mola wetu Mlezi Mtukufu: "Na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri, na kwetu sisi mtarejeshwa" Suratul Anbiyaa: 25

Kheri na shari ni kwa sababu wewe umepewa majukumu, na majukumu ndio lengo la uwepo wako.

Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu "Aliyeumba mauti na uhai ili awatahini nyinyi, enyi watu, ni yupi miongoni mwenu aliye mwema wa matendo na utakasaji wa nia? Na Yeye Ndiye Mshindi Ambaye

hakuna chochote kinachomshinda, Ndiye Mwingi wa msamaha kwa anayetubia miongoni mwa waja Wake" (1) Suratul Mulk.
Na kuwepo kwa shari na kuwepo kwa mitihani na mabalaa, mambo hayo kama yalivyo ni dalili kubwa juu ya usahihi wa swala la dini na kutokuwa sawa kwa upagani.
Tungelikuwa ni watu wa ulimwengu wa kutoamini ila kinachoonekana tusingeweza kutambua lolote si kheri wala shari.
Na ulimwengu wote usingelikuwa na maana.[32]Kwa sababu sisi kulingana na mtazamo wa kipagani tunaishi katika mambo yasiyo ya hiyari tena yenye kuonekana vikali, na unatupitia mfumo wa asili, na kwa mtazamo huu kamwe hatutoweza kuelewa kiini cha shari wala maana ya neno shari.
Hivi viumbe hai wengi wanaelewa mabadiliko ya shari yenye kudhuru?
Kitendo cha kujua kuwa kuna shari, hii inamaanisha kuwa sisi si watoto wa ulimwengu huu, na kuwa sisi tunaongeza maarifa ya uwepo wa shari kupitia vyanzo vingine vya dunia visivyoonekana tofauti na hivi vya Mwanafalsafa (Charles Darwin).
Sisi tunajinasibisha na chanzo kilichoko mbinguni, na wala si katika uvumbuzi wa vitu vyenye kuonekana wa hapa ardhini, na hii ndio tafsiri ya pekee ya kuitambua shari.
Kwa muda wote ambao tunaendelea kubebeshwa majukumu, hivyo ni kawaida kuwa na mitihani na balaa, na ni kawaida kuelewa maana ya shari.
Shari na baadhi ya maumivu na uwezo wa kufanya maasi ni jambo la kawaida na ni matokeo yasiyohitaji kusoma ya kuwa na uhuru wa maamuzi na kubeba majukumu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
Na kuwepo kwa shari na balaa na masaibu na matamanio, mambo haya ndio yanayoweza kutoa kilichoko ndani ya mtu mwema au uovu kwa mtu muovu.
Na laa ajabu katika hali za wapagani wanaposema wakati wa kukanusha kuwa hakuna muumbaji kwa sababu kuna shari, nikuwa wao hutumia suluhisho hili:
1- Mzazi anapokuwa ni mtu wa kheri na anapenda kheri kwa mwanaye, basi ni kwa nini akubali kumchoma sindano yenye maumivu dhidi ya vijidudu?
2- Kuna maumivu yamepatikana kwa mtoto wakati wa kuchomwa sindano?
3- Basi huyo baba ni sawa na hayupo.[33]
Hivi, je, haya yanaweza kutoka akilini kweli!?
Kisha ni kawaida sisi kutoelewa hekima za ndani zaidi za Mwenyezi Mungu katika kheri au shari.
Na alizionyesha wazi Mwenyezi Mungu hekima katika vitendo vya Khidhri kwa Nabii Mussa amani iwe juu yake, pamoja nakuwa ni matendo yanayochukuliwa kwa muonekano ni uovu na hayakubaliki, lakini yamebeba kheri kubwa, na kisa cha Mussa na Khidhri hakikuja ndani ya Qur'ani ili mradi tu kitajwe au kama hekaya (Ngano), bali ni kwa ajili ya mazingatio na kukiri udhaifu wa nafsi ya mwanadamu na kuhukumu kwake mambo haraka haraka.
Na la kushangaza zaidi katika swala la shari nikuwa: Laiti kusingelikuwa na shari kabisa katika ulimwengu basi usingeweza kutoka mahali ulipozaliwa!
Na wala tamaduni zisingelipatikana na miji isingejengwa wala nyumba, na wala watu wasingelihitaji kuwa na kazi, na watu wasingelifikiria kupambana na maradhi au kutatua matatizo au kubuni fikra ya kuleta raha!
Na watu wasingelihitaji kuhama kutoka mahali walipozaliwa kabisa.
Kwa sababu hakuna shari wala hakuna tabu wala balaa wala shida wala matatizo unayoweza kuyatafutia ufumbuzi!
Kwa nini unapata tabu na kukesha na kufikiri na kufanya kazi?
Hivyo, shari ni dharura ambayo ni lazima tuwe nayo ulimwenguni!
Basi, hebu tafakari!
Na muogope Mwenyezi Mungu hakika wewe umepewa majukumu.
Na watu wengi hufikwa na balaa na shari wakarudi kwa Mwenyezi Mungu na wakawa ni watu wema, ametakasika Mwenyezi Mungu na sifa njema ni Zake.
Mipango ya Mwenyezi Mungu yote inahekima na kheri ndani yake.
Na ni lazima muislamu aamini makadirio yote ya Mwenyezi Mungu, amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Na laiti ungelikuwa na dhahabu kubwa mithili ya mlima Uhudi (Uko katika mji wa Madina) ukautoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu asingeliupokea kutoka kwako mpaka uamini

---

[32] C. S. Lewis.
[33] Rejea kitabu Ususul ghaaibah, cha M. Ahmad Hassan, cha kituoa cha Dalaailu. Wao kama wahusika.

mipango na kadari, na ujue kuwa yaliyokufika hayakuwa ni ya kukukosa, na yaliyokukosa hayakuwa ni ya kukupata, na bila shaka atakaye kufa akiwa nje ya imani hii ataingia motoni"[34].
Mipango na kadari za Mwenyezi Mungu kama kheri na shari ni wajibu kwa muislamu kuridhia.
Na kadari zote za Mwenyezi Mungu ni heri, hata kama itaonekana katika baadhi yake kuwa ni shari au dhiki au maudhi kwa muonekano, lakini mwisho zimebeba heri kubwa na hekima za Mola Mlezi za hali ya juu.

## 31- Je, dini imesababisha vita vya udini vilivyoenea katika ardhi kwa kipindi kadhaa?

Jawabu: Wanadamu waliishi katika sheria ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa maelfu ya miaka, na pamoja na sheria tatu kubwa za nabii Ibrahim kwa miaka elfu nne, na dini haikuwahi kusababisha hatari ya moja kwa moja kwa jinsia yoyote ya wanadamu bali iliwaletea watu thamani ya maadili ya hali ya juu wanayokubaliana kwayo waumini na wapagani, na ikaleta ustaarabu tangu mwanzo, bali tunaweza kusema kuwa kila zuri juu ya ardhi ni matokeo ya utume huo! Dini imezipumzisha mahakama kwa maelfu ya kesi, na juu ya zaidi ya hilo nikuwa dini imeweka misingi ya kufahamiana kitabia na kimaadili kwa kukamilisha lengo la kuwepo mwanadamu juu ya ardhi! Na nchi zilizolinda sheria hii ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu bado mpaka sasa kupishana kwa maadili kumebaki kwa wapinzani wao, na imeweka paa la kuwahami kwa mujibu wa sheria ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu kama ipasavyo, kwa wakati ambao karne moja inapokaribia baadhi ya nchi za wapagani basi watu wote huwa katika ukingo wa maangamivu! Kisha leo hii wanakuja wapagani kutueleza hatari ya dini kwa mwanadamu! Historia ya mwanadamu haijawahi kujua mfumo hatari kama upagani, kwani hayakuwa mauaji ya halaiki ya collage katika muungano wa nchi za Sovieti uliopita ila ni kwa mikono ya mpagani Lenin, na mauaji ya kikabila huko Ujerumani, na kuwaondoa robo ya wakazi wa Kambodia katika ubinadamu kwa mikono ya mpagani Pol Pot, na mauaji ya wachina milioni hamsini na mbili (52M) katika mapinduzi makuu ya utamaduni yaliyofanywa na Mao Zedong, na kudhihiri kwa mtandao wa kijeshi wa wapagani (League of Militant Atheists) huko Ulaya uliozifungia rasmi taasisi za kidini takriban elfu arobaini na mbili (42,000) -Makanisa na Misikiti-, na ukaua makumi ya maelfu ya watu wa dini, isipokuwa wenye itikadi ya upagani, na yakawa ni matokeo ya kuenea kwa upagani.[35]Bali hata vita mbili kuu za dunia ya kwanza na ya pili zilikuwa ni vita vya kipagani, vilikuwa vikitawaliwa na mitazamo ya upagani kwa jinsia zote za binadamu, na mitazamo ya kusafisha ukoo, matokeo yake yakawa ni kuangamiza karibu asilimia 5% ya wakazi wa ulimwengu, na vita vikawarudisha nyuma kimaendeleo wote walioshinda na walioshindwa vita kwa takriban theluthi ya karne, na wanafalsafa wakaanza kuweka maeneo ya kukidhi haja ndogo kati kati ya mji wa Paris ikiwa ni fumbo la kumaanisha mwisho wa ustaarabu (Maadili). Na vita hivi vya kipagani vikaacha ghala kubwa la silaha za nyukilia za kutosha kuangamiza binadamu wote kwa mara zaidi ya moja. Hata ufuatiliaji mdogo wa vita vya karne hii ya ishirini unaonyesha wazi matatizo ya upagani. Upagani uliacha nyuma yake fikra ya kuwamaliza binadamu kwa vita yoyote ijayo kuwa ndio fikra endelevu, na haya ndio matokeo ya upagani yaliyotarajiwa.

## 32- Ni kwa nini waislamu wako nyuma pamoja nakuwa dini yao ni ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu wakati ambao wamagharibi wako mbele mno katika maendeleo?.

Jawabu: Hili ndio swali la kuhusu tamaduni!
Ni mara ngapi wamepata tabu Manabii katika kukabiliana na swali hili.
Na ni mara ngapi walikengeuka wafuasi kwa sababu ya jambo hili.
Swali la tamaduni ndio chanzo cha ukafiri wa umma zote kwa zama zote.
Alisema Mwenyezi Mungu Mtukufu "Na watu wakisomewa Aya zetu zilizoteremshwa zilizo wazi, wale waliomkanusha Mwenyezi Mungu wanasemakawaambia Waumini, «Ni pote gani kati yetu na nyinyi lenye mashukio bora zaidi na makalio mazuri zaidi?» Suratu Maryam: 73. Na zikisomwa Aya ambazo zina hoja na dalili za wazi juu ya usahihi wa dini, makafiri hutoa hoja ya hatua ya maendeleo ya makafiri "Lipi katika makundi mawili lenye cheo kizuri na lilio bora barazani?"
Anasema mtafiti Ibrahim Assukrani -Mwenyezi Mungu amuhifadhi-: "Na hii ni kanuni ya kihistoria na ni mfumo wa ulimwengu wenye kujirudia, maajabu hayamaliziki kwa mwenye kuzingatia kumbukumbu zake zenye kumaliza umri, jopo la wafikishaji kutoka kwa Mwenyezi Mungu tangu kuchomoza kwa utume

[34] Sahihi Sunan Abii daud, 4699.
[35] https://en.wikipedia.org/wiki/League_of_Militant_Atheists

mpaka kipindi cha kazi ya Uislamu cha sasa wanakabiliana daima na "Nguvu ya mali" kufaulu kwao na watu kufitinika na kuacha kufuata wahyi (ufunuo) walionao.
Na tazama uzoefu wa Manabii, utakuta unakaribia kuwa wote ni mfano wa kitu kilichochongwa chenye kuzungumza, ambacho ni kwa ajili ya mapambano kati ya mfikishaji "Ufunuo wa Mwenyezi Mungu" na mtihani wa "Nguvu ya mali", Utakuta ni namna gani watu wamefitinika na nguvu ya mali inawavuta wasomi wake na inawakwepesha kutosikiliza na kujisalimisha kuukubali ufunuo, na utawakuta wenye kufanya kazi ya dini wanataabika na machungu ya aina mbili, watu kufitinika na mandhari yenye kuonekana. Mtume wa kwanza ni Nuhu amani iwe juu yake, watu wake walisema kumwambia wazi kuhusu swala la mali: "Wala hatukuoni wamekufuata ila wale waliokuwa kwetu watu duni (Masikini). Suratu Hud: 27 Haukupita muda akajitokeza Nabii Mussa na ukajirudia upya muendelezo wa ubabe wa kutumia mamlaka na kuhadaika mbele ya ufunuo. "Na Musa akasema; Mola wetu Mlezi! Hakika wewe umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali katika maisha ya dunia. Hivyo wanapoteza watu katika njia yako." [88] Surat Yasin. Na hali haikuwa ngeni kwa Nabii wetu Muhammadi -Rehema na amani ziwe juu yake- walikuwa wapingaji wa utume wake na ufunuo alionao wakishikilia katika kumpinga madhaifu yake ya kiuchumi. "Na hawa washirikina wa Kikureshi walisema, «Iwapo hii Qur'ani inatoka kwa Mwenyezi Mungu kikweli, basi si ateremshiwe mtu mkuu kutoka miji hii miwili" (Makkah au Ṭāif). Suratuz Zukhruf: 31.
Mwisho wa kunukuu maneno ya Ibrahim Al-ssukran.
Kwa zama zote na historia ya utume daima binadamu hawajawahi kupewa mtihani mkubwa kuliko mtihani wa nguvu ya kiuchumi kwa kafiri.
Pamoja nakuwa hakuna mahusiano kabisa kati ya maendeleo na haki.
Hivyo, maendeleo ya kiuchumi na kudorora hayana mahusiano na mtu mwenye haki au batili.
Si lazima mtu kuwa mbora au mwema mpaka awe na maendeleo ya kiuchumi.
Mtu anaweza kushikamana na mafundisho ya Uislamu lakini ni masikini wa kati, na inaweza kuwa kinyume.
Ni umma ngapi zilikuwa na maendeleo nao wakawa ni watu wako mbali zaidi na sheria ya Mwenyezi Mungu na dini yake na wahyi wake "Je hawatembei katika ardhi wakaona ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Nao walikuwa na nguvu zaidi kuliko wao, na wakaitimbua ardhi na wakaistawisha zaidi kuliko walivyoistawisha wao." [9] Suratu Rum. Hivyo, maendeleo ya kiuchumi na utajiri wa mali si kipimo cha mtu mwenye haki. "Walipowajia, hao ummah waliowakanusha, Mitume wao kwa dalili zilizo wazi, walifurahia, kwa ujinga wao, ujuzi walionao unaogongana na yale waliyokuja nayo Mitume, na ikawashukia wao ile adhabu waliokuwa wakiiharakisha kwa njia ya shere na dhihaka. Katika aya hii kuna dalili kuwa kila ujuzi unaogongana na Uislamu au kuutia kombo au kutilia shaka usahihi wake, basi ujuzi huo ni mwenye kutukanika na kuchukiza, na mwenye kuuamini si miongoni mwa wafuasi wa Muhammad, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukie". Suratu Ghafir: 83.
Hivyo, mwenye maendeleo ya kiuchumi hana sifa nzuri kupitia hali yake, lakini pia hana ubaya kwa sababu ya hali yake, bali husifiwa kulingana na kiwango cha kuutukuza ufunuo wa Mwenyezi Mungu, na kwa kiwango cha kuifanyia kazi dini, na kwa kiwango cha wewe kunufaika naye katika dini yako, na kwa kiwango unachoweza kumtumia katika kuwanufaisha watu na kurekebisha hali zao kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu.
Na haya ndio maendeleo yanayotakiwa.
Kipimo cha kuzidiana ubora cha uhakika kati ya watu hakiko katika maendeleo yao ya kiuchumi lakini ni kwa kuzidiana katika uchamungu na matendo mema, na yanakuja maendeleo ya kiuchumi kama njia na si lengo kuu, yaje kama njia ya kupata huduma na kuwanufaisha watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.
Maendeleo ya kiuchumi hutakaswa na wahyi wa Mwenyezi Mungu, nao pekee ndiyo maendeleo yanayotakiwa.
Na hii ndio maana halisi ya kuitawala ardhi: Kuitawala kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu, na kuzitawala kila nyanja za maisha kwa utakaso wa imani. "Wale tuliowaahidi kuwa tutawanusuru ndio wale tukiwapa utulivu kwenye ardhi na kuwatawalisha humo kwa kuwapa ushindi juu ya adui wao, wanasimamisha Swala kwa kuiitekeleza kwa nyakati zake kwa namna zake, wanatoa Zaka za mali zao kuwapa wastahiki wake, wanaamrisha kila ambalo Mwenyezi Mungu Ameliamrisha la haki Zake na haki za waja Wake na wanakataza kila ambalo Mwenyezi Mungu Amelikataza na Mtume Wake. Na ni wa Mwenyezi Mungu Peke Yake mwisho wa mambo yote, na mwisho mwema ni wa uchamungu". Suratul Haji: 34. Na tambua kuwa muislamu akitekeleza majukumu yake basi Mwenyezi Mungu humfanyia wepesi sababu za furaha na mazuri yote na maendeleo katika dunia, na kufaulu na kunyanyuliwa daraja Akhera. "Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini miongoni mwenu na wakafanya matendo mema kwamba atawarithisha ardhi ya washirikina na atawafanya ni wasimamizi wa hiyo ardhi, kama alivyofanya kwa waliokuja kabla

yao kati ya wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, na Aifanye Dini yao ambayo Ameridhika nayo na Akawachagulia, nayo ni Uislamu, ni Dini yenye ushindi na uthabiti, na Azigeuze hali zao kwa kuwaondolea hicho na kuwaletea amani, iwapo watamuabudu Mwenyezi Mungu, Peke Yake, na watasimama imara kwa kumtii, na wasimshirikishe na kitu chochote. Na Mwenye kukanusha baada ya hilo la kupewa usimamizi, amani, uthabiti na utawala kamili, na akakanusha neema za Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waliotoka nje ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu". Suratun Nur: 39.
Na wakati wowote waislamu watakapotekeleza dini yao basi watakuwa viongozi katika dunia na akhera.
Na Uislamu umewaletea ustaarabu uliodumu kwa miaka 1200 ukiwa ni utamaduni uliodumu kwa muda mrefu zaidi bila kusimama au kukatika muda wake.
Uislamu uli ulianzisha maendeleo ya kiislamu.
Na maendeleo haya yanapatikana ndani ya dini hii iliyo anzisha ustaarabu.
Dini zilizobakia zililelewa na tamaduni tofauti tofauti.
Utakuta tamaduni za Magharibi zimelelewa na Ukristo, na tamaduni za Kihindi zimelelewa Kihindusi.
Ama dini pekee iliyoanzisha tamaduni ni Uislamu.
Waislamu wanapotambua wajibu wao upande wa dini yao basi wataiongoza dunia kiuchumi na kiroho.
Na Uislamu ulipoingia Costantin (Uturuki) mwaka 1453 A.D, zama za giza za kati zilimalizika Ulaya.
Historia ya kumalizika zama za giza ni mwaka 1453 A.D, na ndio mwaka huo huo ambao Uislamu uliingia katika bara la Ulaya.
Ghafla baada ya kuingia Uislamu Ulaya ikaenea ndani yake nuru ya elimu.
Na katika Maktaba kubwa ya baraza la Congress kumechorwa juu ya paa la ukumbi mkuu wa Maktaba mviringo unaoonyesha vyanzo vya maendeleo ya Magharibi, na Uislamu ndio dini ya kwanza kutajwa katika mizunguko hiyo saba.
Uislamu ndio dini pekee iliyotajwa, nayo imehusishwa na elimu ya mazingira.
ISLAM: PHYSICS
Wakati ambao mizunguko mingine inahusiana na majina ya miji, na michango ya miji hii ni maendeleo ya taaluma au fani au lugha!.
Uislamu umeitangulia Sayansi kwa zaidi ya Miaka mia saba (700) lugha ya kimataifa ya maswala ya Sayansi ilikuwa ni lugha ya Kiarabu[36]
Watakapo itengeneza waislamu dini yao basi itatengamaa dunia yao.

# 33- Ni yapi matokeo chanya ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu?

Jawabu: Mwanadamu alivyoumbwa yeye mwenyewe hajijui uhalisia wake na wala roho yake haipati utulivu wala wasi wasi wa moyo wake hautulii isipokuwa kwa kumuabudu Mwenyezi Mungu "Na Anawaongoza wale ambao nyoyo zao zimetulia kwa kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kumtaja zikapata utulivu. Jua utanabahi kwamba kumtii Mwenyezi Mungu, kumtaja na malipo mema kutoka Kwake yanafanya nyoyo zitulie na zipumbae". Suratur Ra'd: 28. Kupitia ibada moyo hutulia. "Na kwa kweli, tunaujua unyongekaji wa kifua chako, ewe Mtume, kwa yale wayasemayo washirikina kuhusu wewe na kuhusu ulinganizi wako. (97) Basi zitukuze sifa (Himdi) za Mola wako na uwe miongoni mwa wenye kusujudu (98) Na muabudu Mola wako Mlezi" Suratul Hijri: 97-98.
Muabudu Mola wako Mlezi: Yaani: Ili moyo wako upate kutulia.
Na ndio maana rakaa mbili anazozisali mja kwa utulivu na unyenyekevu huleta athari kubwa ndani ya nafsi ya mwanadamu kwa kiwango ambacho hakuna kikao cha kutuliza nafsi kinaweza kufikia kiwango hicho.
Ibada ndani yake kuna liwazo la nafsi, na mtu yeyote aliye mbali na kumkumbuka Mwenyezi Mungu lazima awe na dhiki ya moyo, utamkuta daima akiipaparikia dunia, hana unyenyekevu wala utulivu. "Na mwenye kupuuza ukumbusho wangu basi atakuwa na maisha ya dhiki" Suratu Twaha: 124.
Na vyovyote vile atakavyokuwa mwanadamu katika riziki pana ila kama hana imani lazima atakuwa na maisha ya dhiki, na atakuwa katika maumivu ya kichwa endelevu yasiyojulikana muda wa kumalizika kwake kwa kutaka kushindana na watu wengine, utamuona daima mwenye msongo.
Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Itakayekuwa dunia ndio hitajio lake Mwenyezi Mungu humsambaratishia jambo lake, na huuweka umasikini wake mbele ya macho yake, na haiwezi

[36] Rejea tovuti ya:
https://www.telegraph.co.uk/news/science/science-news/3323462/Science-Islams-forgotten-geniuses.html

kumjia dunia isipokuwa kile alichoandikiwa, na itakayekuwa Akhera ndio dhumuni lake, basi Mwenyezi Mungu humkusanyia jambo lake, na huuweka utajiri wake moyoni mwake, na dunia humjia ikiwa dhalili"[37].
Ibada inamuacha huru muislamu na kuinyenyekea dunia, na inamfanya kuwa huru.
Na ndio maana muislamu mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu ipasavyo ndiye mwanadamu aliyefahamu vizuri maana ya uhai, na kafahamu thamani ya dunia, na kafahamu lengo la kuwepo kwake katika ulimwengu huu, na kafahamu kuwa yuko katika ulimwengu huu kwa kupewa mtihani na ili amuabudu Mola wake ukweli wa kumuabudu na si kua aishi katika msongo usiokuwa na utatuzi, amesema Mtukufu: "Aliyeumba mauti na uhai ili awatahini nyinyi, enyi watu, ni yupi miongoni mwenu aliye mwema wa matendo na utakasaji wa nia? Na Yeye Ndiye Mshindi Ambaye hakuna chochote kinachomshinda, Ndiye Mwingi wa msamaha kwa anayetubia miongoni mwa waja Wake" (2) Suratul Mulk.

# 34- Ni yapi yanayodhihirisha kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu? Au kwa namna nyingine: Utafahamu vipi kuwa wewe umejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kikamilifu?.

Jawabu: Alama za kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni nne nazo ni:
Ya kwanza: Ni utumwa kwa Mwenyezi Mungu katika kila dogo na kubwa katika maisha yako, Amesema Mtukufu. "Sema, ewe Mtume, kuwaambia hawa washirikina, «Hakika Swala yangu na nusuk yangu, yaani kuchinja kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Peke Yake; Pia uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe wote". «Asiye na mshirika katika uungu Wake wala katika Umiliki Wake wala katika majina Yake na sifa Zake. Kumpwekesha huko Mwenyezi Mungu kulikosafishika ndiko Alikoniamrisha mimi Mola wangu, Aliyetukuka na kuwa juu. Na mimi ni wa kwanza kumfuata Mwenyezi Mungu kikamilifu katika umma huu.» Suratul An-am: 162-163.
Swala zangu na vichinjwa vyangu na uhai wangu na mauti yangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu: Kila kitu ninakifanya kwa jili ya Mwenyezi Mungu, Mimi nina swali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na nina watii wazazi wangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na ninarejea masomo yangu na kujifunza ili niwanufaishe watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na nina lala ili nipate nguvu kesho ya kufanya yale aliyo niamrisha Mwenyezi Mungu.
Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu katika kila jambo, na hii ni katika alama muhimu ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu.
Alama ya pili ili uweze kujisalimisha kamili kwa Mwenyezi Mungu: Ni kuyafuata aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu na kuyaepuka aliyoyakataza, amesema Mola wetu Mtukufu: "Enyi ambao mlimuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kuweni na utiifu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake katika yale Aliyowaamrisha kwayo na Akawakataza nayo, na msiache kumtii Mwenyezi Mungu na kumtii Mtume Wake na hali nyinyi mnazisikia hoja na dalili zinazosomwa kwenu kwenye Qur’ani". Suratul Anfal: 20.
Amesema Aliyetakasika na kutukuka: "Enyi mlioamini ingieni kwenye amani wazima wazima" Suratul Baqara: 208.
Amani yaani: Uislamu.
Ingieni katika amani wazima wazima: Yaani Shikamaneni na yote aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu na yaacheni aliyoyakataza.
Ameniamrisha Mwenyezi Mungu jambo nilifanye, na kanikataza jambo niliache, na huku ndiko kujisalimisha kamili na kutii kwa Mwenyezi Mungu.
Alama ya tatu ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu: Ni kujisalimisha kwa kuhukumu kwa sheria alizoziweka Mwenyezi Mungu, turidhie sheria zake na tuzikubali.
Tunazikubali sheria zote za Mwenyezi Mungu na wala hatukanushi chochote mfano adhabu alizoziweka Mwenyezi Mungu, bali hatunabudi kuridhia sheria za Mwenyezi Mungu, kwa sababu Mwenyezi Mungu anajua yanayowafaa viumbe wake, na anajua kuwa katika adhabu hizi kuna kuisafisha jamii "Hivi asijiue aliyeumba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari" [Suratul Mulk: 14].
Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na ni nani mwenye hukumu nzuri kuliko Mwenyezi Mungu" Suratul Maida: 50.
Mwenyezi Mungu ndiye anayejua yanayowafaa watu katika dunia yao na katika akhera yao.
Na kuzitekeleza sheria za Mwenyezi Mungu huwasafisha watu na huwafanya watu waishi katika amani.
Mtu mmoja anayedai kumuamini Mwenyezi Mungu na yale yaliyoteremshwa kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- alikwenda kwa Myahudi Ka'bu bin Ashraf ili ampe hukumu katika kesi miongoni

[37] Sahihi Sunanut Tirmidhi, Had: 2465.

mwa kesi badala ya kwenda kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, kwa kuhofia kuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- atahukumu kwa hukumu ambayo yeye haitompendeza, akaenda kwa Yahudi akitaraji hukumu itakayomridhisha, ikateremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Kwani hukujua, ewe Mtume, mambo ya wale wanafiki wenye kudai kuwa wameyaamini yale uliyoteremshiwa, nayo ni Qur’ani, na yale waliyoteremshiwa Mitume kabla yako, ilhali wao wanataka kuhukumiwa, katika ugomvi unaotokea baina yao, kwa sheria ya batili, isiyowekwa na Mwenyezi Mungu, na wao waliamrishwa kuikataa batili? Shetani anataka kuwaepusha na njia ya haki na kuwaweka mbali nayo kabisa". Suratun Nisaa [165]

Ukiwa ni muislamu mwenye kutii amri za Mwenyezi Mungu unawajibika kushikamana na amri za Mwenyezi Mungu, na ukubali hukumu za Mwenyezi Mungu hata kama hukumu ya Mwenyezi Mungu itakuja tofauti na matamanio yako, hupaswi kuacha sheria ya Mwenyezi Mungu na kwenda kwa Myahudi ili akuhukumu katika kesi yako ili tu akuridhishe.

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika aya zilizofuata:

"Na hatukutuma Mtume yeyote isipokuwa atiiwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu" Suratun Nisaa: 64.

Mwenyezi Mungu hakutuma Mitume ili tuachane nao na tukahukumiane katika sheria isiyokuwa yao.

Kisha anahitimisha Mwenyezi Mungu somo katika tukio hili na mfano wake kwa aya muhimu inayobainisha udharura wa kunyenyekea kwa kuhukumiana kwa sheria za Mwenyezi Mungu, amesema Mola wetu Aliyetakasika na kutukuka: "Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Anaapa kwa nafsi Yake tukufu, kwamba hawa hawataamini kikweli mpaka wakufanye wewe ni hakimu kwenye ugomvi unaotokea baina yao katika uhai wako na watake uamuzi wa Sunnah yako baada ya kufa kwako, kisha wasiingiwe na dhiki katika nafsi zao kwa matokeo ya hukumu yako, na wakwandame, pamoja na hivyo, kwa kukufuata kikamilifu. Kutoa uamuzi kulingana na aliyokuja nayo Mtume wa Mwenyezi Mungu, Rehema ya Mwenyezi Mungu na amani zimshukiye, kutoka kwenye Qur’ani na Sunnah katika kila jambo katika mambo ya kimaisha, pamoja na kuridhika na kusalimu amri, ni miongoni mwa uthabiti Imani" Suratun Nisaa: (65)

Hatunabudi kusalimu amri kikamilifu katika yale aliyoyaweka Mwenyezi Mungu kuwa sheria, kusalimu amri katika sheria za Mwenyezi Mungu ni katika alama za utiifu kwa Uislamu!.

Ama alama ya nne ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni: Kujisalimisha katika makadirio ya Mwenyezi Mungu, kila jambo alilolikadiria Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa hekima yake, na hapo muislamu anajisalimisha kwa Mwenyezi Mungu katika makadirio yake yote , katika kheri na shari.

Akifikwa muislamu na yenye kufurahisha hushukuru, na akifikwa na yenye kuhuzunisha husubiri.

Na lau akikuruzuku Mwenyezi Mungu chakula au riziki nyingine nzuri au nyumba nzuri au ufaulu katika masomo au afya katika mwili au familia bora unamshukuru Mwenyezi Mungu.

Na yakimfika muislamu matatizo kama maradhi au ufakiri au hofu au balaa au msongo, anasubri katika matatizo haya na anataka msaada kwa Mwenyezi Mungu, hii ndio hali halisi ya muislamu mtiifu aliyejisalimisha kwa Mola wake Mlezi na Mtukufu.

Kila jambo linakwenda kwa mipango ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: Afya na maradhi na utajiri na umasikini, kila kitu kinakwenda kwa mipango yake na hekima zake, na ni juu ya muislamu kuridhia kadari kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye anayepanga.

Amesema Mola wetu Mlezi Mtukufu: "Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo" Suratul Qamar: 49. Na alisema Allah Mtukufu: "Sema; Kamwe halitufiki sisi isipokuwa aliloliandika Mwenyezi Mungu kwetu" Suratu Ttaubah: 51.

Kamwe, halitotufika ila alilolipanga Mwenyezi Mungu kwetu.

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na haikuwa nafsi yoyote ni yenye kufa ila ni kwa idhini ya Mwenyezi Mungu" [Surat Al Imrani: 85]

Mauti yamekwisha pangwa na Mwenyezi Mungu.

Na kila kinachotokea katika ulimwengu na kila chembe ndogo inayotembea katika ulimwengu na kila tukio linalotokea, bila shaka yanatokea kwa elimu ya Mwenyezi Mungu na matashi ya Mwenyezi Mungu na kwa mipango ya Mwenyezi Mungu na kwa hekima ya Mwenyezi Mungu na kwa uweza wa Mwenyezi Mungu.

Amesema Mola wetu Mlezi Mtukufu: "Na akaumba kila kitu akakiwekea kiwango maalum" (2) Suratul Furqan: 23.

Yeye Mtukufu ameumba kila kitu na akakikadiria kila kitu, ayatakayo huwa na asiyoyataka hayawezi kuwa.

Mimi kama muislamu ninatakiwa kusalimu amri kwa makadirio yote ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na kwa hili ndio mwanadamu anakuwa muislamu.

## Na mwisho kabisa! Nitaingia vipi katika Uislamu?

Uislamu ndio dini ya Mwenyezi Mungu kwa wanadamu wote, Amesema Mtukufu: "Hakika dini pekee mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu" [Surat Al Imrani: 85] Uislamu ndio dini pekee ambayo Mwenyezi Mungu hakubali dini nyingine isiyokuwa hiyo "Na Mwenye kutafuta dini isiyokuwa dini ya Kiislamu, basi hiyo haitakubaliwa kwake, na yeye Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye kupata hasara". [Surat Al Imrani: 85]

Na kwa ajili hii ni wajibu kwa kila mwanadamu aukubali Uislamu.

Ndani ya Uislamu kuna kuokoka na moto na kufaulu kwa kupata radhi za Mwenyezi Mungu na Pepo.

Na kuingia ndani ya Uislamu ni neema katika neema kubwa, bali ndio kubwa na ni kitu muhimu katika uwepo wako.

Na Uislamu uhalisia wake ni kurejea katika maumbile na akili salama.

Na kuingia katika Uislamu ni jambo jepesi mno, wala halihitaji kafara (Tambiko) wala mambo maalum, ni mtu tu kutamka Shahada mbili, nako nikusema: "Ash-hadu anlaa ilaaha Illa llahu Wa ash-hadu anna Muhammadan Rasuulu llaah" Maana yake: Nina kiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi yakwamba; Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mungu Mmoja, na kuwa Muhammadi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Na kwa hili tayari mtu ameishakuwa muislamu.

Kisha anaanza kuufanyia kazi Uislamu.

Nina muusia afuatilia tovuti ya islamhouse.com, kila mmoja kulingana na lugha yake, ili muislamu mpya ajifunze ni namna gani ataufanyia kazi Uislamu.

Kiunganishi cha tovuti ni: https://islamhouse.com/ar/

KUKIMBIA KUTOKA KATIKA UPAGANI KWENDA KATIKA UISLAMU.

1- Nini maana ya upagani?
2- Ni kitu gani mnacho kiona ni dosari katika upagani?
3- Ni upi ushahidi wa kuwepo kwa muumbaji?.
3- Nini maana ya ushahidi wa kuleta?
5- Nini maana ya ushahidi wa kujali na ufanisi?
6- Kwa nini asiwe mwanadamu na viumbe vinginevyo vyanzo vyao vya mwanzo ni malighafi ndogo kabisa?
7- Ni ipi mifano ya kuonyesha ushahidi wa kutilia manani na ufanisi?
8- Baadhi wa pagani hupinga ushahidi wa kutiliwa manani na kusema kuwa kuna baadhi ya vitu si ukamilifu, mfano: Kama maradhi, na matetemeko?
9- Ni kipi kinachozuia kuwa ulimwengu ulipatikana kwa sababu nyingine yenye kushikika au kuonekana; Mfano: Kama ustaarabu mwingine au kitu kingine chochote? Kwa nini awe ni Mungu wa tangu pekee?.
10- Sisi twazifahamu kanuni zinazo uendesha ulimwengu, na tunazijua sababu za matetemeko ya ardhi vizuri, kwa nini tuhitaji muumbaji wakati tushazijua kanuni?
11- Ni kipi kinazuia kuwa chanzo cha dunia ni ghafla (kama ajali)?.
12- Vipi tunaweza kumjibu mpagani anayesema kuwa ulimwengu ni wa tangu?.
13- Ni kwanini haizingatiwi kanuni ya sasabu kwa muumbaji? Au kwa maelezo mengine: Ni nani aliyemuumba muumbaji?
14- Ulimwengu ni mkubwa; Inawezekanaje kwa miili yetu hii midogo tuwe kituo cha ulimwengu huu mpana kiasi hiki?
15- Wanasema baadhi ya wapagani: Ziko sayari nyingi sana, na hivyo, kwa mujibu wa nadharia ya "Uwezekano wa asili" yawezekana kukawa na Sayari katika Sayari hizo inayowezekana watu kuishi ndani yake. Je, ni sahihi kuleta ushahidi huu?
16- Kwa nini kusiwe na muumbaji zaidi ya mmoja wa tangu?
17- Kwanini Dini?
18- Kipi kinazuia maadili na tabia hizi kuwa ni matokeo ya akili za watu au jamii fulani?
19- Kuna miungu wengi katika tamaduni mbali mbali za ulimwengu, ni kwa nini iwe imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu tu?
20- Ikiwa mtu atafanya jambo ambalo halihitaji basi huu ni mchezo! Na Mwenyezi Mungu hana haja na sisi, hivyo, ni kwa nini alituumba?
21- Tutamjua vipi Mwenyezi Mungu?
22- Kuna dini nyingi sana, kwa nini iwe Uislamu pekee?
23- Uislamu ni nini?
24- Je katika Uislamu kuna majibu ya maswali yaliyotatiza akili nyingi kuyajibu: Tulitoka wapi? Na kwanini sisi tuko hapa ulimwenguni? Na tunaelekea wapi?
25- Nimejuaje kuwa Muhammadi -Rehema na amani ziwe juu yake- ni Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu?
26- Ninawezaje kujua kuwa mimi ninatakiwa kumuamini Mwenyezi Mungu?
27- Je, inatosha kumwamini Mwenyezi Mungu na kuwapinga Manabii?
28- Je kafiri anapata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya matendo yake mema?
29- Ikiwa Uislamu ni dini ya haki kweli, kwa nini kunapatikana utata ndani yake?
30- Kwa nini Mwenyezi Mungu aliumba shari? Au kwa maana nyingine: "Anajibu vipi muislamu kuhusu shari yenye kutaabisha"?
31- Je, dini imesababisha vita vya udini vilivyoenea katika ardhi kwa kipindi kadhaa?
32- Ni kwa nini waislamu wako nyuma pamoja nakuwa dini yao ni ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu wakati ambao wamagharibi wako mbele mno katika maendeleo?.
33- Ni yapi matokeo chanya ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu?
34- Ni yapi yanayodhihirisha kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu? Au kwa namna nyingine: Utafahamu vipi kuwa wewe umejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kikamilifu?.

Na mwisho kabisa! Nitaingia vipi katika Uislamu?